Gazeti la kwanza la Islam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

Nukuu ya Qur'an Tukufu

Na Hatuwatumi Mitume ila wawe watoaji wa habari njema na waonyaji. Na wale waliokufuru wanajadili kwa uwongo ili kwayo waibatilishe haki; na wakazifanya Aya Zangu na yale waliyoonywa kuwa mzaha. (Al Kahf: 18:57)

JUZU 82 No. 228 | SAFAR - JAM.I 1443 AH | JANUARI 2022 | TAB.-FAT 1400 HS | BEI TSH. 500/=

Ujumbe wa Khalifa kuhusu mwaka mpya



Khalifa Mtukufu (atba) Aliwahutubia wanajumuiya duniani kote kwa hotuba yake ya Ijumaa iliyotolewa tarehe 31-12-2021 kutoka Masjid Mubarak U.K. na mwishoni mwa hotuba yake alisema kuwa mwaka mpya unaanza kesho na Aliomba, Mwenyezi Mungu aufanye mwaka huu mpya kuwa wenye baraka kwa Jumuiya na wanajumuiya wote. Jumuiya ihifadhiwe na maovu yote, na njama zote dhidi ya Jumuiya hii zisifanikiwe. Na tuwe miongoni mwa wanaoshuhudia utimilifu wa ahadi aliyoitoa Mwenyezi Mungu kwa Masihi Aliyeahidiwa (as).

Khalifa Mtukufu (atba) alisema kwamba tunapaswa kuingia katika mwaka mpya kwa maombi. Tahajjud inapaswa kuswaliwa,na misikiti mingi inapanga kwa ajili ya hili. Wale ambao bado hawajapanga mipango wafanye hivyo. Ikiwa haiwezekani kusali katika jamaa, basi watu wanapaswa kusali Tahajjud mmoja mmoja majumbani mwao na waendelee kufanye maombi mengi na wajijengee na tabia ya namna hii kwa siku zote.

Khalifa Mtukufu (atba) alisema kuwa pamoja na Durood Sharif [sala juu ya Mtume (saw)] na Istighfar [kuomba msamaha], dua zifuatazo zapaswa kusomwa:

Endelea uk. 4

Matawi manne ya Dar es salaam yafanya maadhimisho ya Siratul Nabi



Amir na Mbashiri Mkuu, Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry akitoa hotuba ya kufungia Maadhimisho ya Siratun Nabi

Tarehe 2 Jan 2022 matawi manne ya Mkoa wa Dar es salaam yamefanya maadhimisho ya SIRATUL NABI. Yaani siku ya kumkumbuka Mtume Mtukufu Muhammad s.a.w. Mgeni Rasmi akiwa Amir na Mbashiri mkuu wa Tanzania Mh Tahir Ahmad chaudry sahib

Maadhimisho hayo yalifanyika Masjid Salaam chini ya usimamizi wa Rais wa Tawi la Mnazimoja. Matawi mengine yaliyoshiriki ni Keko ambaye Rais wake ni Bw Omari kilimo. Tawi la Safina ambaye Rais wake ni Shams Shoo na Temeke Mikorshini Rais wake ni Ally Mwihaji.

Sherehe ilianza kwa usomaji wa Quran Tukufu Sura Muhammad kunzia aya ya kwanza mpaka 12 na msomaji ambaye alitoa tafsiri baadaye pia ni Mwl Ashraf Ndembo. Baada ya hapo mwenyekiti wa kikao bw Mohamed Yunus Haji amlikaribisha Mwl Isihaka Nyamihasi kusoma Shairi ambalo linamsifu Mtume Mtukufu Muhammad s.a.w Salle Allah Muhammad salle Alaihi wasalli Muhammad muongozi, ndiye yetu kiongozi. Aloleta nuru hizi,ndiye mpenzi wangu mie.

Baada yake katibu wa Tawi la mnazimoja alikuja kusoma masharti ya baiat na kutoa maelezo kidogo kuhusu masharti hayo.

Kikao kilendelea ambapo pia Rais wa Mkoa bw Saidi Mgeleka alikuwepo na baraka zake tumezipata Ndipo mwenyekiti alikaribisha Mwl Adam kutoa Hotuba juu ya Maisha ya Mtume Mtukufu Muhammad s.a.w. Alianza kwa kusoma tashahud na kumsomea Mtume na Akianza kwa kusema, Siratul Nabii ni siku ambayo tunajikumbusha Maisha ya Mtume Mtukufu s.a.w , maisha ambayo ni mfano mwema kwetu (33:22) kila hatua ya maisha yetu tunapata mfano kutoka maisha yake. Utajiri, Umasikini, maisha ya ujana na utu uzima ndoa na kadhalika, kupitia yeye ndiyo tunaweza kumpata Allah(3:32) kwa hiyo Siratul Nabii inatujuzu kufanya mara kwa Mara ili kuweza kujikumbusha maisha yake na tumfuate mfano wake ambayo kwetu ni ya lazima tuishi kama alivyotufundisha na ikiwa tunampenda Allah subhana hu wa ta'ala

Masihi a.s ni ujio wake wa pili wa Mtume Mtukufu Muhammad s.a.w hivyo kila mwanajamati anatakiwa atambue kwa kumpokea Masih Ahmad a.s na awajibike kuishi maisha ya kiislam sawa na mafundisho yaliyoletwa na Mtume Mtukufu s.a.w na kufundishwa tena katika zama hizi na Masihi wake Sayyidna Ahmad a.s

Hotuba ya pili ilitolewa na Mwl Nasoro kisusa iliyohusu

Endelea uk. 8

Ufahamu mpango wa Waqf-e-Jadid uk. 4

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

KIAPO

Katika nchi nyingi siku ya kuapishwa kwa Kiongozi Mkuu ni siku ya shamra shamra nyingi na matumaini makubwa kwa wananchi. Ni siku ambapo kiongozi anafanya ahadi yeye na nafsi yake kuwa anayatoa maisha yake kuwatumikia watu. Na ushahidi wa jambo hili ni kitabu kitakatifu anachokiamsha kwa mkono wake wa kulia.

Lakini kula kiapo ni nini, na nini umuhimu wake? Kula kiapo kwa maana na matumizi maarufu ya kiapo ni kuishuhudisha nafsi ya mtu au imani yake juu ya ukweli wa jambo ambalo ushahidi wa kawaida haupatikani. Pia ni ahadi ya dhamira ya kutekeleza kwa nguvu zako zote na maarifa yako yote jambo hilo ulilokubaliana kulitekeleza. Hivyo unaposikia kuwa Rais, makamo wa Rais, Waziri mkuu, Spika na wateuliwa wengine wote wanaapishwa, hilo sio jambo dogo hata kidogo. Hiyo ni ahadi kwa aliyekuumba na ni ahadi kwa viumbe wake pia kwamba utatekeleza wajibu kwa imani ya kuwa ingawaje wewe humuoni, Mwenyezi Mungu, Yeye Anakuona.

Ni jambo la hatari kubwa kulichukulia jambo hili kwa mzaha, lakini wapo waliotoa machozi wakati walipokabidhiwa madaraka wakiuliza nafsi zao iwapo wangeweza kutimiza wajibu waliopewa ipasavyo.

Siku ya kuapishwa ni siku ngumu sana, hivyo kabla hujashika kitabu kitakatifu mkononi mwako na kuapa mbele ya Mwenyezi Mungu ni muhimu kuiuliza nafsi yako: Je nimeheshimu na kufuata kanuni zote zilizotakiwa, je nimepokea rushwa, nimefanya dhuluma, ni kweli nimeshinda katika uchaguzi huu? Haya maswali hakuna wa kuyajibu isipokuwa wewe mwenyewe binafsi. Ni jambo linaloumiza na linalotetemesha nafsi; wewe unajua kabisa ulifanya kila hila katika kuchafua mkondo wa haki, halafu kwa ujasiri, tena ujasiri usiofaa, unaapa mbele ya Mwenyezi Mungu kwamba utashika haki na kuomba kwamba akusaidie; lakini akusaidie katika nini, je umesahau uliyofanya? Hivyo kabla hujakula kiapo ni vyema usafishe nafsi yako kwanza, ndipo Mwenyezi Mungu akusaidie, kwani Mwenyezi Mungu haingii mahala pachafu. Ukishajihakikishia kwamba umejikagua, sasa hapo ndipo unaweza kushika kile kitabu ukiaminicho kwa ni kitakatifu kuapa kutekeleza hayo ambayo cheo chako kinakutaka uyatekeleze.

Kwa kiapo hiki, uelewe kwamba umeingia katika mkataba na ile nguvu isiyochoka, isiyolala, na inayoendelea kufuatilia nyayo zako, na ule msaada ulioomba utapatikana tu iwapo utatekeleza majukumu yako kwa nia na shabaha ya kupata radhi ya Mwenyezi Mungu.

Tatizo kubwa linalotukabili ni kutokuwa na viongozi wanaokumbuka viapo vyao. Kinachotawala fikra zao ni kuwasiadia ndugu zao hata kama hawastahili, kukusanya pesa kwa ajili ya uchaguzi ujao, hivi tutapata lini nafasi ya kufikiria ufumbuzi wa matatizo ya watu kama wakati wote tutawaliwa na fikra za uchaguzi ujao?

Maradhi haya ya kusema tusiyoyatenda, yanajenga ganzi miongoni mwa wananchi, mara nyingi wao wanasema bila kusema, wanapiga makofi, kumbe nyoyo zao zinaungua. Na usidhani wamesahau, kauli za viongozi wanazo wameziweka kwenye makabati ya nyoyo zao, ni kujidanganya kufikiri kuwa wamesahau.

Hivyo ni muhumu kuwa waangalifu na yale tunayoyasema. Mshairi mmoja alisema kweli aliposema:

“Nakuasa usikie usemayo ni karama, maneno usirukie, sema mambo kwa kupima.”

Ukiwa kiongozi lazima uwe mwangalifu na kauli zako. Ukiwa kiongozi, umepwa amana ya kuweka siri kama kiapo chako kinavyosema kwamba hutatoa siri nje, na hii yote inatawaliwa na mtu yule ambaye anamuhofu Mwenyezi Mungu na anelewa kwamba kesho kuna maswala ya kujibu.

Kiapo ni ahadi, ahadi ya kutimiza wajibu wako katika kulitumikia taifa, ni heshima kupewa nafasi ya kutumikia taifa lako, sio wengi wanaopata heshima hiyo. Basi tafadhali usiichafue heshima hiyo!



QUR'AN TUKUFU

Sura An Nas

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيمِ

Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa Ukarimu.

قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ الْفَلَقِ.

Sema: Najikinga kwa Mola wa mapambazuko,

مِن شَرِّ مَا خَلَقَ.

(Anilinde) katika shari ya alivyoviumba,

وَمِن شَرِّ غَاسِقٍ إِذَا وَقَبَ.

Na katika shari ya giza la usiku liingiapo,

وَمِن شَرِّ النَّفَّاثَاتِ فِي الْعُقَدِ

Na katika shari ya wale wanaopulizia mafundoni,

وَمِن شَرِّ حَاسِدٍ إِذَا حَسَدَ

Na katika shari ya hasidi anapohusudu.

NUKUU YA HADITHI

وَعَنْ عَلِيٍّ رَضِىَ اللّٰهُعَنْهُ قَالَ قَالَ رَسُوْلُ اللهِ صَلَّى اللّٰهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يُوْشِكُ اَنْ يَّاْتِىَ عَلَى النَّاسِ زَمَانٌ لَا يَبْقَى مِنَ الْاِسْلَامِ اِلَّا اسْمُهٗ وَلَا يَبْقٰى مِنَ الْقُرْاٰنِ اِلَّا رَسْمُهٗ، مَسَاجِدُ هُمْ عَامِرَةٌ وَهِىَ خَرَابٌ مِنَ الْهُدٰى عُلَمَآءُ هُمْ شَرُّ مَنْ تَحْتَ اَدِيْمِ السَّمَآءِ مِنْ عِنْدِهِمْ تَخْرُجُ الْفِتْنَةُ وَفِيْهِمْ تَعُوْدُ۔ (رواه البيهقى فى شعب الايمان)

Imesimuliwa na Hazrat Ally r.a. ya kwamba mjumbe wa Allah*saw* alisema: ni karibu iwadie juu ya watu zama ambapo hakitabaki chochote cha Qur'an isipokuwa maandishi yake.(katika zama hizo) misikiti yao itaendewa (kidhahiri) na watu wengi lakini itakuwa mitupu upande wa mwongozo, maulamaa wao watakuwa wabaya sana kuliko wowote walio chini ya mbingu. Kutoka kwao fitina itatokea na itawarejea wao wenyewe.

(Kukipitia Mishkat, Kitabul Elm, Hadith no.263)

ASEMAVYO MASIHI ALIYEAHIDIWA*as*

Kusali nyuma ya asiye Ahmadiyya

Seyyidna Ahmad as. ameandika kwamba "wakufurishaji na wakadhibishaji ni wafu tu. Kwa hiyo hawafai, mwanajumuiya yeyote asisali nyuma yao. Je, mzima anaweza kusali nyuma ya mfu? Basi kumbukeni kwamba Mungu Ameniambia kwamba ni haramu juu yenu na ni haramu kabisa kwamba msali nyuma ya mkufurishaji, mkadhibishaji na mwenye shaka yeyote. Bali inapaswa kwamba Imamu wenu awe miongoni mwenu. hiyo ni dalili inayopatikana katika Hadithi ya Sahihi Bukhari kwamba امامكم منكم (yaani amamu wenu awe miongoni mwenu.)"

(Dhamima Tuhufa Golarwia, Ruhani Khazain jal. 17 uk 64 Hashia) cha 1900 AD

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Dr. Swaleh Kitabu Pazi
Kompyuta: Ahmad Abdul Nasibu.
Mchapishaji: Sheikh Raghib Zia ul Haq
Msambazaji: Mwl. Omari Ali Mnungu
Wajumbe:
1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga
2. Mahmood Hamsin Mubiru.
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu36@gmail.com

Maisha ya Mtume Muhammad *saw*

Yalivyosimuliwa na Hadhrat Mirza Bashir ud Din Mahmud Ahmad r.a. Khalifatul Masih wa pili wa Masihi Aliyeahidiwa[as]

Inaendelea Kutoka toleo lililopita

KUHAMIA MADINA TOKA MAKKA

Mtume s.a.w. na wenzake walianza matayarisho ya kuhama. Familia moja baada ya nyingine ikaanza kutoweka Makka na hata wale watu waliokuwa wakiusubiri ufalme wa Mungu nao pia wakapata ujasiri. Wakati mwingine ndani ya siku moja tu, nyumba za mtaa mzima wa Makka zilikutwa zikining'inia kufuli. Na baada ya Alfajiri watu wa mjini walipoukuta mtaa ukiwa kimya, walipouliza wakafahamu kuwa watu wote wa mtaa huu wamehamia Madina na baada ya kuiona athari hii kubwa ya Islam iliyokuwa ikienea ndani kwa ndani miongoni mwa watu wa Makka wakawa wanastaajabu. Hatimae Makka kukawa hakuna Waislamu. Wakawa wamebakia tu watumwa wachache, Mtume s.a.w. mwenyewe, Hadhrat Abu Bakar r.a. na Hadhrat Ali r.a.

Watu wa Makka walipoona kwamba sasa mawindo yanatuponyoka, basi viongozi wakakutana tena na kuamua hivi baada ya kushauriana kwamba sasa kinachostahili kufanywa sasa ni kumuua tu Muhammad s.a.w.

Kwa fadhili makhsus za Mwenyezi Mungu, tarehe ya (njama za kutaka) kumuua zikawa zimeafikiana na tarehe za kufanya kwake Hijra. Wakati watu wa Makka walipokuwa wakikusanyika nyumbani kwake kwa ajili ya kumuua, yeye, ndani ya giza la usiku, alikuwa akitoka nje ya nyumba yake kwa dhamira ya kufanya Hijra. Bila shaka watu wa Makka walikuwa na mashaka kwamba huenda habari za njama zao zilikuwa zimeshamfikia Muhammad s.a.w. Lakini hata hivyo alipopita mbele yao, wao wakadhani hivi kuwa huyo pengine atakuwa ni mtu mwingine na badala ya kumshambulia wenyewe wakaanza kujificha wasionekane ili habari ya dhamira yao isije ikamfikia Muhammad s.a.w.

Siku moja kabla ya usiku huu Hadhrat Abu Bakar r.a. pia alikuwa kishapewa habari ya kushiriki naye katika Hujra hii. Hivyo akakutana naye pia na wote wawili wakakutana na ndani ya muda mfupi tu wakaondoka Makka na wakakimbilia kwenye pango la mlima Thaur uliokuwa maili tatu nne hivi nje ya Makka.

Watu wa Makka walipotambua kuwa Muhammad s.a.w. ameshaondoka Makka, basi wakakusanya jeshi fulani na kuanza kumfuatilia. Wakamchukua pia mtaalamu fulani wa kufuata nyayo ambaye, kwa kuzifuata alama za nyayo zao, wakafika hadi kwenye mlima wa Thaur. Baada ya kufika kule kwenye pango alikokuwa (Mtume s.a.w.) amejificha pamoja na Abu Bakar r.a., (mtaalamu) yule akasema kwa yakini kabisa kwamba aidha Muhammad s.a.w. yumo ndani ya pango hili au atakuwa amepaa mbinguni.

Moyo wa Abu Bakar r.a. ulipoyasikia maneno yake haya ukashikwa na hofu kubwa na akaanza kumwambia Mtume s.a.w. kwa sauti ya chini kwamba: Adui ameshakaribia kabisa na sasa wakati wowote ule ataingia pangoni. (Mtume s.a.w.) akamwambia Laa tahzan Inna Laaha ma'anaa yaani usihofu ewe Abu Bakar, Mungu Yu pamoja nasi. Abu Bakar r.a. akasema: Ewe Mtume wa Allah! Mimi siihofii nafsi yangu, kwani mimi ni mtu tu wa kawaida, nikifa itakuwa ni mtu mmoja tu amekufa. Ewe Mtume wa Allah, hofu yangu ilikuwa hii tu kwamba kama uhai wako upate shida yoyote ile, basi jina la dini na utawa vitatoweka duniani. (Mtume s.a.w.)akasema usijali, hapa hatuko wawili, bali wa tatu wetu Yuko pia Mwenyezi Mungu.

Kwa kuwa sasa wakati ulikuwa umeshafika kwamba Mwenyezi Mungu Aikuze Islam na kuipa maendeleo na wakati wa muhula kwa ajili ya watu wa Makka ulikuwa umeshamalizika, Mwenyezi Mungu Aliweka pazia machoni mwa watu wa Makka nao wakaanza kumkejeli yule mtaalamu wa kufuata nyayo na kumwambia kwamba: Je ilikuwa aje kweli kujificha kwenye eneo lililo wazi namna hii, hii sio sehemu ya makimbilio. Na halafu kwenye sehemu hii kuna nyoka na nge wengi, nani awezaye kukimbilia sehemu hii? Hivyo badala ya kuchungulia pangoni wakamcheka mtaalamu yule na kurudi walikotoka.

Baada ya kusubiri ndani ya pango hili kwa siku mbili, sawa na mipango il;iyokwisha amuliwa hapo kabla, wanyama wa kusafiria wakaletwa kule pangoni majira ya usiku na Mtume s.a.w. na wenzake wakasafiri kwa kutumia ngamia wawili waendao kasi. Ngamia mmoja alipandwa na Mtume s.a.w. na mwenye kuongoza njia na ngamia wa pili alipandwa na Hadhrat Abu Bakar r.a. na mtumishi wake Aamir bin Fuhaira.

Kabla ya kuelekea Madina, Mtume s.a.w. aliuelekeza uso wake upande wa Makka, mji ule mtakatifu aliozaliwa, ambamo alipewa utume, ambamo mababu kwa mababu zake walikuwa wakiishi humo tangu zama za Hadhrat Ismail a.s., aliutazama kwa mara ya mwisho na kuutamkia mji huo akiwa na huzuni kwa kusema: Ewe mji wa Makka, mimi nakupenda wewe zaidi kuliko sehemu zote, lakini watu wako hawaniruhusu kuishi hapa.

Wakati huo, Hadhrat Abu Bakar r.a. naye pia akasema kwa huzuni kwamba: Watu hawa wamemfukuza nabii wao, sasa hao ni lazima wataangamia.

Ufunguzi wa Msikiti wa Maenje

"MASJID KARIM" - MKOANI RUKWA

Mnamo tarehe 21-11-2021, Jumuiyya ya Waislamu wa Ahmadiyya mkoani Rukwa, ilifanikiwa kufanya ufunzuzi wa msikiti katika kijiji cha Maenje, Mwambao wa ziwa Rukwa, wilaya ya Rukwa vijijini.

Kwa fadhili za Allah msikiti huu ulipata bahati kubwa ya kufunguliwa na sheikh wa kanda ya nyanda za juu kusini Maulana Sheikh Karim Uddin Shams sahib, anaesimamia mikoa ya Mbeya, Songwe, Rukwa na Katavi.

Sheikh sahib, aliwasili mkoani Rukwa katika kijiji cha Maenje Mwambao wa ziwa Rukwa mnamo majira ya saa 6:30 adhuhuri akitokea Mbeya ambapo Mbeya alitoka asubuhi saa 12:30. Akiwa ameongozana na Qaid Khuddamul Ahmadiyya Mkoa wa Mbeya bw. Shaban Suleiman Juma, pamoja na khuddam wengine wawili. Umbali wa kutoka Mbeya mpaka Rukwa ni kama km 300 hivi.

Mara baada ya kuwasili tu, Sheikh sahib, alilakiwa na rais wa jamaat wa mkoa wa Rukwa bw. Mohammed Lugoya, ambaye alifuatiwa na mwl. Wa jamaat ya Maenje mwl. Bashir. H. Mrope - akifuatiwa na wanajamaat na wasiokuwa wanajamaat wote waliungana kwa pamoja kumpokea Sheikh sahib.

Ilipotimu saa 7:30 vionzozi wa serikali waliokuwa wamealikwa wote walikua ndo wanaingia na hivyo watu wote walisogea na kukusanyika mbele ya msikiti tayari kabisa kwa kusubiri zoezi zima la ufunguzi wa msikiti, muda ulipowadia utaratibu ulikuwa kama ifuatavyo, mstari wa mbele kabisa alikuwepo Sheikh sahib, waalimu wa Jamaat, yaani mwl. Bashir Mrope na mwl. Makarani Balama, kisha viongozi wa serikali yaani afisa mtendaji, mwenyekit na Mwalimu wa shule ya msingi.

Zoezi la kukata utepe liliongozwa na Sheikh sahib, pamoja na afisa mtendaji, wao wawili walisogea mlangoni msikitini na kwa pamoja walikata utepe na takbira zikasomwa kwa wingi na mwl. Makarani Hamza na wote walioshuhudia tukio hilo wakajibu kwa sauti kubwa Allahu Akbar.

Mara baada ya kumalizika zoezi la kukata utepe, Sheikh sahib aliwaongoza wanajamaat wote na wasiokuwa wanajamaat katika maombi ya pamoja na ya kimya, huku akiwatangazia wale wasiokuwa wanajamaat kuwa maombi yetu hufanywa kimya kimya na kila mtu anaweza kuomba kwa imani yake na kwa lugha yake.

Baada ya kumalizika kwa maombi watu wote waliingia msikitini wakiongozwa na sheikh sahib, aliyefungua mlanzo wa msikiti na kutangulia kuingia kisha watu wote wakaingia na mara tu baada ya watu wote kuingia, Adhana ilisomwa na mwl. Makarani Hamza Balama, na Sheikh Karim Uddin sahib akaongoza sala za Adhuhuri na Alasir.

Mara tu baada ya sala, mkutano / kikao rasmi cha ufunguzi wa msikiti kikaanza. Na mkutano ulianza kwa usomaji wa Quran Tukufu, iliyosomwa na mwl, Makarani Hamza Balama. Yeye alisoma sura 2:126-130. Baada ya usomaji wa quran ilifuatiwa na maneno machache ya namna ulivyopatikana msikiti yaliyowasilishwa na rais wa mkoa wa Rukwa bw. Mohammed Lugoya, ambapo yeye alisema: mpaka hii leo, umepatikana msikiti katika jamaat ya Maenje viging vingi sana vimerukwa na wanajamaat wa hapa Maenje, miongoni mwa vigingi hivyo ni, kutangatanga sehemu ya kufanya ibada maana wakati huo hata eneo yaani uwanja wa kujenga msikiti haukuwepo, hivyo kila sehemu tuliyokuwa tunaipata kwaajili ya kufanyia ibada mwisho wa siku tulifukuzwa.

Sehemu ya kwanza kabisa ilikuwa ni ya kijana mmoja aliyekuwa amejiunga, (familia ya ntinda) hapa tulisali ijumaa moja, ilipokuja ijumaa ya pili mzazi wa huyu kijana akasema tafuteni sehemu nyingine ya kuswalia maana mimi sitaki majini katika nyumba yangu, hivyo wale wanajamaat wote waliojiunga hali ilikuwa hivyo hivyo katika majumba yao yote, kisha ikaonekana kuna shule ambayo imetoka tu kujengwa na madarasa yapo tu, basi ijumaa ikahamia kule shule ya msingi, ambako nako ilisaliwa ijumaa moja tu nako ikasemekana shule itakapofunguliwa wanafunzi wataanza kudondoka kwa sababu ya majini ya hawa Waislam hivyo nako ijumaa ikahama tena na ndipo mwanajamaat moja akaamua atoe mti wake wa muembe uliokuwa na kivuli kizuri kwa ajili ya kufanyia ibada zote hapo, zikiwemo sala za ijumaa. Mwanajamaat huyo ni bw. Suleiman Kadius.

Ibada zote ziliendelea hapo, mpaka pale tulipofanikiwa kununua uwanja wa jamaat ndipo tena tulipohama kwenye mti wa muembe mpaka kuhamia kwenye mti wetu eneo la uwanja wa Jamaat, huku zikikusanywa nguvu za wanajamaat za kufyatua matofali ili ujenzi wa msikiti uanze mara moja. Hivyo rais alisema mpaka leo hii msikiti umesimama ni kwa msaada mkubwa saana wa Mwenyezi Mungu.

Na ikumbukwe ya kuwa nguvu ya awali ya ujenzi wa msikiti huu ni ya hawahawa vijana wapya waliojiunga kutoka ukristo kwani walifanya kazi ya kujitolea kwa juhudi zote ili kuhakikisha tu msikiti unasimama, na kwa msaada wa Allah vijana walifyatua matofali na kuzichoma na kwa kusaidiwa nguvu kutoka kwa Sheikh wa kanda mnamo mwaka 2018 msikiti ulijengwa na kuezekwa bati msikiti wenye ukubwa wa futi

Waqf-e-Jadid

Kutoka toleo Lililopita

Na **Sheikh Karimuddin Shams**

Chuo cha kwanza cha Walimu:

Hakukuwa madrasa maalum kwa ajili ya kuwaanda walimu mwanzoni. Wataallamu wa Jamaat walikuwa wanawafundishia walimu katika "Masjid Mubarak" kwa muda wa miezi miwili tu na miongoni mwa Wataallamu wake, walikuwemo Hazrat Mirza Tahir Ahmad r.a., Maulana Abul Muniir Noorul Hak Sahib, Maulana Abu-ul-Ata Sahib, Maulana Jalal-ud-din Sahib Shams,na Seyyed Zain-ul-Abediin Shah Sahib kisha Hazrat Maulana Ghulam Rasool Sahib Rajeki aliwafundishia baadhi ya mambo ya tiba ya kiasili na hazrat Mirza Tahir Ahmad r.a. aliwafundishia mambo ya msingi na muhimmu kuhusu tiba ya "Homeopathy" na katika mwezi wa pili mwaka 1958, hivyo wakfiin 14 walichaguliwa na kufundishwa kwa muda wa wiki moja na mnamo tarehe mosi ya February 1958 walimu sita walitumwa matawini kisha wakfiin 22 walifanyiwa usaili na kuchaguliwa mnamo Februari 16 hivyo basi hadi mwisho wa mwaka wake wa kwanza vituo 90 vilikuwa vimeshaanza shugli zao. (Khulafae ahmadiyyat ki Tahrikat uk.235)

Kazi ya tanziim hiyo ilipoanzishwa tu watu kadhaa walipata kujiunga na Jamaat kutokana na mpango huu adhimu wa Wakfe Jadid na pamoja na shuguli za maelezi na mahubiri vijijini, mahubirir kwa wasio Waislam pia yalifanyika hasa na Wakfe Jadid na baadhi ya watu walijitolea mashamba yao kwa ajili ya mpango huu na hadi zama za khalifa wa pili kuna mashamba hecta 700 yalikuwa yameshatolewa na wanajamaati.

Kwa ajili ya kuimarisha shuguli zake, idara kadhaa kwa majina ya Nizamat ziliundwa na mainspecta (wakaguzi)na Muhasseliin(makatibu wenye kukusanya mchango) pia waliteuliwa kwa majukumu ya kupokea ahadi na mchango kwa wakati. Ikumbukwe kuwa mchango wa kwaida hutolewa na wale tu wanaokuwa na kipato ndani ya Jamaat ila mchango wa Wakfe Jadid inatolewa na wanafamilia wote hata wasio na kipato.

Watu elfu sita waliweza kutoa mchango wa Wakfe Jadid katika mwaka wake wa kwanza na hivyo mpango huu wenye baraka tele ulianza safari yake na kuendelea kupata mafanikio makubwa mwaka hadi mwaka na mpaka mwisho wa zama za ukhalifa wa pili walimu 71 walikuwa wanaendelea kuitumikia Jumuiyya na kazi ya mahubiri na malezi ilikuwa inaendelea katika vituo 64.

Wakfe Jadid Duniani Kote

Mwanzoni mpango huu ulianzishwa kwa ajili ya Pakistan, India na Bangladesh tu na mnamo mwaka 1986, khalifa wa nne r.a. aliupanua katika nchi zote ili watu wa nchi zingine pia washiriki kwenye mpango huu na kupata baraka zake.

Kwa sasa kuna maelfu ya walimu wanaendelea kuitumikia dini katika vituo vingi mno na kuna chuo maalum kwa ajili ya walimu nchini Pakistan, kiitwacho "Madrasa tuz Zafar" kinachotoa huduma na zaidi ya mia walimu wanajifunza pale kila mwaka na wakufunzi 13 pamoja na Mwalimu mkuu wanaendelea kufundisha, kuna hosteli(bweni) tena ipo cha hadhi kabisa, kisha kuna madrasa kuu nchini India na Bangladesh halafu nchi kadhaa zina vyuo vyaa walimu ambavyo haipungui 10 ikiwemo nchi yetu Tanzania ingawa kwenye vyeo hivi, mpango wa Tahrike Jadid pia unatoa mchango mkubwa kwa ajili ya kuviendesha.

Kila mwalimu anakuwa na jukumu la kuwalea na kuwafundishia wanajamaati kwenye matawi yake pamoja na kufanya mahubiri yaani anasimamia shuguli za kufundisha sala, yassar nal Kuran, Kurani Tukufu, Tafsiri ya Kurani na kuchunguza kuwa wanajamaati wangapi husali sala tano kila siku, wangapi wanashiriki katika kutoa mchango, wangapi wasikiliza hotuba ya Khalifa wa zama n.k. hivyo basi shuguli nzima za mahubiri na malezi ni jukumu lake mwalimu.

Mgawanyiko wa Mchango wa Wakfe Jadid;

Mwaka wa Wakfe Jadid unaanza tarehe mosi ya January kila mwaka na kuishi tarehe 31 ya Decemba. Wanajamaati, wakubwa kwa wadogo, wakina mama kwa wakina baba, wasichana kwa wavulana wote wanashiriki katika Wakfe Jadid na kutoa michango yao kwa mgawanyiko huu:

1. Mchango wa Wakfe Jadid Baleghan (watu wazima)
2. Mchango wa Wakfe Jadid Atfal o Nasirat (wavulana na wasichana)
3. Kyam e Marakaz (kuanzisha vituo)
4. Imdad Marakaz (kutoa msaada kwa ajili ya vituo)

Daftar Atfal:

Khalifa tul Masih wa Tatu hazrat Hafiz Mirza Nasir Ahmad r.a. alitangaza mpango maalum kwa ajili ya Watoto mnamo 7 Octoba 1966 unaoitwa Daftar Atfal naye alisema akiwahutubia watoto wa kiahmadiyya wenye umri wa miaka 15 kwamba:

"Leo,ningewaomba Watoto (wasichana na wavulana) wa kiahmadiyya kuwa; Enyi Watoto wa Mungu na Mtume Wake, simameni na kusonga mbele na kuziba pengo lililopatikana kwenye shuguli za Wakfe Jadid kutokana na uzembe wa wazee wenu. (Al-Fazal 12 Octoba 1966)

Homeo Dispensary:

Kuna dhahanati ya kutumia tiba ya Homeopathy, iliyoanzishwa mnamo 1960 chini ya Wakfe Jadid nchini Pakistan, inayoendelea kutoa huduma zake hadi leo na wastani watu 200 wanaopata matibabu huko kila siku lakini kwa msaada wa Mwenyezi Mungu kuna vituo vingi mno ambavyo vinatoa huduma hii duniani kwani walimu wa Wakfe Jadid pia wanatoa huduma ya kuwatibu wagonjwa kuipitia tiba ya Homeopathy.

Khalifa tul Masih wa Tatu hazrat Mirza Nasir Ahmad r.a. alisema akiwaelekezea wanajamaati kwenye majukumu yao kwamba;

"Wakati ule, hazrat Musleh Maud r.a. alihisi kuwa kuna haja ya kupeleka mwalimu katika kila tawi…Jumuiyya inyewe inahisi kwamba majukumu yao, yaliyojuu yao kuhusu malezi ya wanajamaati hayatekelezwi kama ipasavyo bila kuwa na mwalimu pamoja nao."(Hotuba ya Ijumaa ya 7 Octoba 1966).

Khalifa tul Masih wa Tano hazrat Mirza Masroor Ahmad A.T.B.A. anasema kuwa:

"sasa ni wakati kwamba; inatakiwa kuwa na Mwalimu au Murabbi katika msikiti wa kila kitongij, kila kijiji, na kila mji. Wanajamaati wanatakiwa kujitolea dhabihu ya mali kwa vyo vyote vile, ndipo tutaweza kufanya hivyo(na kupeleka mwalimu kwao).. watalazimika kutoa dhabihu ya Watoto wao (kuwa Wakfiin), kwa ajili ya shuguli hii. Na hao wote wawe wenye kushika vipimo vya juu vya ucha-Mungu, hatutawapelekea tu Watu(walimu) bali wenye kushika ucha-Mungu wanahitajika…. haja ya watu(walimu) inaendelea kuongezeka kwa fadhila za Allah Taalah. Mwenyezi Mungu, Aendelee kutupatia walimu na Masheikh, wenye kushika Ucha-Mungu.

Kwa ajili ya kukamilisha na kutimiza kusudio na lengo la kuanzishwa kwa Wakfe Jadid, tuna hitaji walimu wengi sana mno pamoja na dhabihu kubwa za mali.

Yakini juu ya mafanikio wa Mpango huu:

Ningependa kumaliza Makala hii kwa maneno yeneye baraka tele za mwanzilishi wa mpango huu wa Wakfe Jadi, hazrat Mirza Bashi ud din Mahmood Ahmad r.a. huzur anasema kuhusu ufaulu na kufanikiwa kwa mpango huu kuwa;

" kazi hii ni ya Mwenyezi Mungu, na lazima itatimia tu kwa kuwa Mwenyezi Mungu Amenifunulia kuhusu Mpango huu hivyo basi lazima nitautimiza hata kama nalazimika kuuza nyumba zangu. Kama hatanisaidia hata mtu mmoja tu miongoni mwa wanajammati, Mweyezi Mungu Atawatenganisha nami ambao hawanisaidii na kuteremsha Malaika toka mbinguni kwa ajili ya kunisaidia mimi."

(Al-Fazal ya January 7, 1958.

Allah Mtukufu Atujaalie sisi sote kuwa wenye kujitolea dhabihu ya kila namna kwa ajili ya kuufanikisha mpango huu kisha kujitolea kwetu kikubaliwe na Mungu Mwenye Enzi na kumridha kama ipasavyo. Amiina (Karim-ud-din Shams).

Mikoa 10 inayoongoza kwa uchangiaji wa Waqf-e-Jadid 2021 Tanzania

(kwa asilimia)

MKOA	WAMELIPA %
Morogoro	128
Tabora	121
Mbeya	111
Dar-es-salaam	105
Iringa	104
Arusha	101
Songea - Ruvuma	99
Mtwara & Lindi	83
Tunduru	74
Tarime - Mara	61

Ujumbe wa Khalifa kuhusu mwaka mpya

Kutoka uk. 1

رَبَّنَا لَا تُزِغْ قُلُوْبَنَا بَعْدَ اِذْ هَدَيْتَنَا

وَهَبْ لَنَا مِنْ لَّدُنْكَ رَحْمَةً اِنَّكَ اَنْتَ الْوَهَّابُ

"Mola wetu, Usiipotoshe mioyo yetu baada ya kutuongoza, na Utupe rehema kutoka Kwako, hakika Wewe ndiwe Mpaji Mkuu. (3:9)

رَبَّنَا اغْفِرْلَنَا ذُنُوْبَنَاوَاِسْرَافَنَا فِىْ اَمْرِنَا

وَثَبِّتْ اَقْدَامَنَا وَانْصُرْنَا عَلَى الْقَوْمِ الْكَافِرِيْنَ

"Mola wetu, Tughofirie madhambi yetu na kupita kwetu kiasi katika mambo yetu na uiimarishe miguu yetu na Utusaidie juu ya watu makafiri." (3:148).

Tunawatakiwa wasomaji wetu wote wanaopatikana duniani kote, heri nyingi na baraka tele za mwaka mpya. Aamin.

Ufafanuzi kuhusu uchawi [Imani za kishirikina]

بسم الله الرحمان الرحيم
نحمده ونصلى علي رسوله الكريم وعلي عبده
المسيح الموعود عليه السلام

KWA MUJIBU WA QUR'AN KUNA AINA MBILI ZA SIHR [MAZINGAOMBWE

Uchawi huu ni wa kufikirika [imagination] na wa dhana tu ambao umetajwa katika Quran kwenye matukio ya Hadhrat Musa [as] na watu wa Firauni waliokusanywa pamoja siku waliyokuwa wameahidiana.

Wa pili ni yale mazingaombwe ya makundi ambayo yanataka kudanganya watu kwa njama na kushawishi pamoja na kueneza uvumi katika Jamii kwa ajili ya kushusha hadhi na heshima ya serikali na kuiasi. Uchawi huu pia umeelezwa kwenye sura Al Falaq.

MAANA YA NENO SIHIR [UCHAWI]

SIHIR; neno hili kwa kiswahili lina maana hizi mbili moja kiini macho, na mbili ni uchawi. Katika lugha ya kiarabu SAAHIR lina maana nyingi kama linavyo elezwa hapa kuwa neno hilo sio kila mara liwe na tafsiri ya mchawi pia lina maana sita zingine zinazo patikana kwenye kamusi ya Akrab na Lane.

1 Mlozi.
2 Mtu anayeliwaza na kutumbuiza.
3 Mtu anayejua, stadi mwenye akili.
4 Mtu mwenye uwezo wa kukifanya kitu kionekane namna nyingine kuliko hasa kilivyo.
5 Mdanganyaji
6 Mlaghai

Katika kamusi ya lisaanul Arab iliyo andikwa na Al-Azhar ame toa maana ya neno Assihr'' kuwa na maaana ya kulibadilisha jambo mbali na uhakika wake, nako ni kuwadhihirishia watu jambo lisilo la kweli wakaliona kuwa ni la kweli.''

Sahaba wa mtume Hadhrat Ibn Abbas [r.a] anasema kuwa ''*uchawi ni kudhihirisha batili katika sura ya haki*''

Hapa tunaona sahaba wa Mtume ambaye aliombewa na mtume [saw] ALLAHUMMA FAKKI HUL QUR'AN [Yaani Eee Allah mfungulie maarifa na elimu ya Qur'an] sasa basi tunaona kuwa kudhihirisha batili katika sura ya haki ni uchawi. Hizo ni maana za wazi kuhusu neno uchawi hivyo tunajifunza kuwa uchawi si kitu chenye nguvu za kisiri na kuweza kumloga mtu , bali ni udanganyifu wa kielimu kuhusu kitu Fulani na kukifanya watu wakione tofauti.

Neno hilo sio kila mara liwe na tafsiri ya mchawi pia lina maana sita zingine zinazo patikana kwenye kamusi ya Akrab na Lane. Neno hili limetumika mara 42 ndani ya aya 41 za Quran likiwa na maana tofauti tofauti na InshaAllah nitaeleza baadhi tu ya aya ili kuweka wazi zaidi na hasa wakati wa kuwafahamisha waislam juu ya imani hii ya ushirikina.

Aya ambazo neno sihir au saahir limetumika ni hizi zifuztazo [2; 10] [5; 111] [6;8] [7;110] [7;114] [7;117] [7;121] [7;133] [26;154 na 186] [61;7] [74;25] hizi ni chache tu kati ya aya 42 nilizo zitaja.

LILIVYO TUMIKA NDANI YA QURAN.

Neno hili lilivyo tumika ndani ya Quran lime maanisha uongo ,udanganyi ,ughiribu na hasa pale nabii wa Allah anapo tumwa kwa watu na kuwaeleza ishara Fulani ushahidi una patikana katika Quran kuwa wao walipo waambia watu wa mwamini mungu waka anza kuwaita wao wachawi. Mfano sura ya 61;7 Na alipo sema Issa mwana wa Mariam; Enyi wana wa Israeli ,mimi ni mtume wa Allah kwenu ,ni sadikishaye yaliyo mbele yangu katika taurati na kutoa habari njema ya Mtume atakaye kuja nyuma yangu jina lake ni Ahmad ; lakini alipo wafikia kwa ishara zilizo wazi,wakasema huu ni udanganyifu dhahiri. 10;77-78 Basi ilipo wafikia haki kutoka kwetu wakasema; huu ni uchawi dhahiri. Akasema Musa ; Je mnasema hivi juu ya haki ilipo wafikieni, Je huu ni uchawi? Na wachawi hawastawi[yaani hawafaulu] 10;81-82 Basi walipofika wachawi ,Musa akawaambia; Tupeni mnavyo taka kuvitupa. Na walipo vitupa, Musa akasema; mlivyoleta ni udanganyifu tu wa macho; hakika Allah hivi karibuni Ataubatilisha. Hakika Allah Hastawishi vitendo vya waharibifu 20;70-71 Na kitupe kilicho katika mkono wako wa kuume; kita vimeza walivyo vitengeneza; hakika wametengeneza hila za mchawi hatafaulu popote. Basi wachawi wakaangushwa kusujudu, wakisema, Tumemwamini Mola wa Harun na Musa.

NUKTA KADHAA ZA KUKUMBUKA HAPA

1 Katika sura ya 61 aya ya 8 ime elezwa kwamba pindi alipo wajia kwa ishara zilizo wazi waka sema huu ni udanganyifu dhahiri, kwa nini waseme udanganyifu ;kwa sababu hawakuelewa ishara zile kwa kung'ang'ania mila zao za zamani na kuchukua mambo yao ya udanganyifu kwa njia mbalimbali hivyo waka muweka Nabii kwenye daraja kama lao wakidhani kuwa kawashinda katika elimu au utaalam wa mazingaombwe yao. Kumbe wo wameshindwa kujua upi uongo na upi ukweli kulingana na jamii yao walio kuwa wanaishi walizungukwa na watu wasio mtambua Mungu na wamejikita kwenye udanganyifu kwa kupata manufaa ya kidunia tu.

2 Huu ndiyo mtazamo tunao ishi nao leo katika karne ya 15 tangu Quran ilipo teremshwa , kwani waislam wengi wamejikita katika kutafuta maisha ya dunia kwa njia yeyote ile na hasa udanganyifu kwa kutumia aya za Quran vibaya na Hadithi za Mtume[s.a.w] kama sehemu ya kujifichia kwa wale wasio jua dini ili wapate kuwadanganya na kufanya wanacho taka. Hivyo unakuta watu wana acha kumwamini Allah kisawasawa wana amini maombi ya sheikhe tu yanatosha.

HADITHI ZA MTUME [S.A.W] JUU YA SHIRKI

Imesimuliwa na Ibn Mas'oud [r.a] ya kwamba Mtume s.a.w alisema hirizi ni shirk,hirizi ni shirki, hirizi ni shirki maneno haya aliyatamka mara tatu.[Abuu dawuud kitaab tibbi baab tayyarah].

Sasa katika jamii tunazo ishi sasa jambo hili limekuwa la kawaida na watu wana imani nalo sana kwamba hirizi inaweza mkinga mtu na balaa Fulani na hasa watoto wana vishwa ili waweze kulindwa na watu wenye uchawi kama inavyo sadikika, ilhali kitu hicho ni imani potofu na kina mpeleka mtu mbali na Mungu wake. Imani hii imepandikizwa vichwani mwa watu toka karne nyingi zilizo pita kiasi kwamba kwasasa ukimwambia mtu hivyo vitu havisaidii kitu na wala havina maana, basi mtabishana na mtu huyo na hato kubali. Kitendo cha kumvisha mtoto hirizi ndiyo anafundishwa toka utotoni kuwa uchawi upo na anahitaji kujikinga, madhara ya vitendo hivi ni haya kuwa endapo wazazi watazeeka na watoto wao wakapata watoto wale wajukuu wata anza kuwaita bibi au babu mchawi na mwisho wa siku nao wanaenda kwa waganga wa kienyeji kuagua kisha hao waganga wana waambia kuwa bibi yako huyo au babu yako huyo na muda mwingine siyo mjukuu ni mtoto wako wa kumzaa anakuja kukuita wewe mchawi na kupanga njama za kukuuwa.

Imesimuliwa na Hadhrat Abuhuraira [r.a] ya kwamba mtume [s.a.w] amesema, hirizi haina maana, hirizi nzuri ndiyo nzuri, akaulizwa hirizi hiyo nzuri ni nini? Akajibu maneno mazuri ambayo mmoja wenu anasikia.

Hapa mtume saw kaweka wazi kuwa hirizi haina maana ila hirizi nzuri ni maneno mazuri ambayo mmoja wenu huyasikia. Sasa tujiulize kulogana ni maneno mazuri au kuna faida gani na familia ipi iliyo endelea wakawa pamoja kwa kufanya mambo haya?

Itaendelea toleo Lijalo

Kifo Juu ya msalaba? Hoja kumi kutoka kwenye Biblia Takatifu

Kutoka toleo lililopita

3. MWELEKEO WA HURUMA WA GAVANA WA KIRUMI

Wayahudi waliipeleka kesi ya Yesu Kristo kwa Pilato, Gavana wa Kirumi wa Falestinia. Alifanya utafiti wa kisheria na hatimae akatangaza kuwa hakuwa na makosa yaliyokuwa katika mashataka. Aliwaambia.

''*Mtu huyu mmemleta kwangu kana kwamba anapotosha watu, nami tazama nimeamua mambo yake mbele yenu, ila sikuona kwake kosa lolote katika mambo hayo mliyomshitaki*''. Luka 23:14.

Akawatokea way tena, akawaambia mimi sioni hatia yoyote kwake. Lakini kwenu kuna desturi ya mimi kuwafungulia mtu mmoja wakati wa Pasaka, basi mwapenda, niwafungulie mfalme wa Wayahudi? Basi wakapiga kelele tena kusema, si huyu, bali Baraba, naye yule Baraba alikuwa mnyang'anyi. (18:38,40).

Na tangu hapo Pilato akatafuta kumfungua lakini Wayahudi wakapiga makelele wakisema, ukimfungulia huyu, wewe si rafiki yake Kaisari, kila mtu ajifanyaye kuwa mfalme humfitini Kaisari.

Kutokana na nukuu zilizotolewa hapo juu, ni dhahiri ya kwamba Gavana alimuona Yesu asiye na hatia sawa na mashataka ya Wayahudi dhidi yake, alijitahidi kwa uwezo wake kumuachilia lakini Wayahudi walipotia kani kumtaarifu Kaisari huko Roma, alisalimu amri kwao na kumkabidhi Yesu kwao lakini kwa njia ya siri alifanya mikakati ya kumuokoa Yesu. Njozi ya mkewe ilikuwa mbele yake na alimaizi kuwa makuhani walikuwa wamekula njama dhidi yake kwa sababu ya wivu na husuda.

Bustani ya Washairi

WAKATI NDIO HUSEMA

Naanza kwa jina Lako, Ewe Mola mtukuka
Ambaye kwa sifa zako, hakuna anayefika
Afananaye hayuko, kwa wote waloumbika
Wakati ndio husema, si hekima zake mtu

Wakati huu tuliko, Islam yatikisika
Tena haina mashiko, pote yaweweseka
Mamlakani waliko, hawajui pa kushika
Wakati ndio husema, si hekima zake mtu

Katika hili zumbuko, Imam ahitajika
Wa kuipa imariko, dini ya Mola Rabuka
Aondoe choko choko, za wapendao faraka
Wakati ndio husema, si hekima zake mtu

Wakati hutoa mwako, nini kinahitajika
Sawa nalo dhihiriko, ya uma ulipofika
Sababu ya maanguko, husema limepasuka
Wakati ndio husema, si hekima zake mtu

Elimu dini haiko, dhana kasi imeshika
Yamebaki maandiko, maana imetoweka
Visa ndio la shiko, washindana kutamka
Wakati ndio husema, si hekima zake mtu

Wa kuongoza hayuko, kwa wote akasikika
Hivyo kuna mpasuko, wa dini yake Rabuka
Na hilo ndio anguko, Islam imefika
Wakati ndio husema, si hekima zake mtu

Mimi nawapa kumbuko, Mtume alitamka
Mia miaka kamiliko, Mujadid atafika,
Na dini yenye sumbuko, lazima taimarika
Wakati ndio husema, si hekima zake mtu

Hassan Sango (Jange Muqadas, kwenye karatasi)
Dar es salaam

YAKINI

Kikombe kimetakata, kwa nje kinavutia
Kwa kila anayepita, mate anakimezea
Na mimi ningekipata, fuadi ingetulia»
kumbe siri ya maiti, aijuae muosha!

Pamwe na mshika kata, maji anayemwagia
Kimya huwa aina sita, lolote kujisemea
Kila mpenda kubwata, kichwani zimepungua
Akatula omungoma, kamanywa omubambi

Uzuri wenye kumeta, ni ndani kuchungulia
Yaliyomo ni mafuta, au uchafu ajaa
Bila yakini tajuta, katika hino dunia
Tizama nje na ndani, kuupata utulivu

Kaditama hujapata, bileshi wajisumbua
Yakubidi kujikita, kiini kukifikia
Au utaula mwata, janga utajivunia
Na kila mvuna janga, hula pamoja na wake

Mahmood Hamsin Mubiru (Wa Mamba)
Kiwalani - Migombani

VIJANA WANGU

Ninao wengi vijana, Wenye mapenzi na dini
Na imani, waungwana, wenye hima kazini
Wenye kiu za kufana, roho zao ibadani
Rawaombea rabana, Awape Janataini

Shunda Mshundia Wana
Daluni, Tanga

KIPIMO CHA UCHAMUNGU

1. Ukweli nauwandika, Akili inanituma, Jaribu kuyaepuka, Ili upate heshima, Uwasi kuuepuka, Utufike mwisho mwema, Kipimo cha uchamungu, Majaribu ya dunia.

2. Shikamana na sheria, Mwenyezi katuwekea, Kuzingatia sheria, Amri katuwekea, Ole ldvunja sheria, Adhabu katuwekea, Kipimo cha uchamungu, Majaribu ya dunia.

3. Yatakuvunja imani, Haki utaangamia, Usijivishe mwilini, Maradhi ya kuumia, Yatakuvunja imani, Mwishowe kuangamia, Kipimo cha uchamungu, Majaribu ya dunia.

4. Vipimo naviandika, Tega sikio sikia, Usikiapo epuka, Jiweke mbali sikia, Usivutike hakika, Kuwa imara sikia, Kipimo cha uchamungu, Majaribu ya dunia.

5. Huyashona mavazi, Yakubana kuvutia, Na yale mabega wazi, Kifuwa kutuvutia, Na siket'i za uwazi, Kila kona zapitia, Kipimo cha uchamungu, Majaribu ya dunia.

6. Wanatuweka kitanzi, Kuitamani dunia, Tujihadhari wapenzi, Tusitamani dunia, Mbele ya ola Kipimo cha uchamungu, Majaribu ya dunia.

Madumula Ng'amilo

SIRI YA CHAKULA

1. Chakula ni mlo, ule uridhike
Kidogo ukile, tumbo sivimbike
Ushinde ulale, uvivu kushike
Mlo ni faradhi, Kiasi kiliwe.

2. Ule cha nafuu, lishe kilojaa
Dona si pilau, mboga na dagaa
Chai karafuu, soda takuua
Mlo ni faradhi, Kiasi kiliwe.

3. Kula kuhusudu, ndugu takukimbia
Uchoyo si budi, kando utupia
Ulafi kizidi, maradhi ugua
Mlo ni faradhi, Kiasi kiliwe

4. Kula kikuzidi, kipato chujuka
Mwenyewe jifisidi, kula ukishika
Wafanya fisadi, njaa tokutoka
Mlo ni faradhi, Kiasi kiliwe

5. Mlo ni faradhi, Kiasi kiliwe
Ukipata faradhi, kipato kikata
Mungu mkabidhi, akiba kukata
Kwa mlo baadhi, jamaa kupata

6. Leo si pumbaze, kesho ipuuza
Sinia ujaze, machipsi kwa pweza
Njaa si iweze, kesho takuliza
Mlo ni faradhi, Kiasi kiliwe

7.Mlo ni faradhi, Kiasi kiliwe
Uko njaa ule, ukishiba acha
Kimoja usile, vya gharama acha
Wasitani ule, kuzidisha acha

Masihi Omary Kisagwa

SUBIRA

1. Ulimwengu sio wangu, nataabika
Yote mipango ya Mungu, ninatomboka
Wala siko peke yangu, kwenye mashaka
Siijui kesho yangu, nitafikaje?

2. Usiku wangu mrefu, usioisha
Humu ndani ya jokofu, mmenichosha
Ninamuomba Turufu, hatanifisha
Siijui kesho yangu, nitafikaje?

3. Na bado nina subira, navumilia
Nitaupata ujira, ninawambia
Moyo hauna papara, umetulia
Siijui kesho yangu, nitafikaje?

4. Siijui kesho yangu, sina hakika
Mungu kimbilio langu, atakumbuka
Maisha yangu machungu, nimegubikwa
Siijui kesho yangu, nitafikaje?

5. Pamoja na hayo yote, ninakumbuka
Sala ninasali zote, siweziruka
Ninapopata chochote, namkumbuka
Siijui kesho yangu, nitafikaje?

6. Kuna muda ninalia, kama mtoto
Mangumu ninapitia, bila majuto
Na Mungu ninamwambia, mambo mazito
Siijui kesho yangu, nitafikaje?

7. Naendeleza subira, nimenyooka
Ninazisaka ngawira, nitazishika
Naomba bila bakora, ninahenyeka
Siijui kesho yangu, nitafikaje?

8. Na kinachonishangaza, wanaumia
Na wanapata bughudha, kunisemea
Mwenyewe bado nakaza, yatatimia
Siijui kesho yangu, nitafikaje?

9. Chakula changu cha shida, navumilia
Ninashindwa kujidoda, nimepotea
Huwa sinywi hata soda, nawaambia
Siijui kesho yangu, nitafikaje?

10. Nakubali kila hali, nayopitia
Bado ninajikubali, mia kwa mia
Itakwisha hii hali, nangojelea
Siijui kesho yangu, nitafikaje?

11. Tuko watu wengi sana, wenye majanga
Hata kama mkinuna, nakujitenga
Ewe Mungu wangu ona, wananinanga
Siijui kesho yangu, nitafikaje?

12. Nimefikia mwishoni, kuwakumbusha
Nyi wote nduguzanguni, sijapotosha
Usiombe we ni nani, wajizungusha
Siijui kesho yangu, sina mashaka.

Abdalla Kalindima
#CHUMACHAKAVU

SALAMU ZA MWAKA MPYA

Bodi ya Uhariri ya Gazeti letu tulipendalo "Mapenzi ya Mungu" inawatakia heri na fanaka ya mwaka 2022.

Tuendelee kuleta makala na kutoa maoni juu ya gazeti letu.

Tunamuomba Allah Aufanye mwaka huu 2022 uwe wa mafanikio zaidi, Amin.

Misumari

Misumari

Katika kijiji kidogo, mvulana wa miaka kumi aliishi na wazazi wake. Kijana huyu alikuwa na tabia mbaya.

Angekasirika kwa urahisi sana na mara nyingi alirusha hasira. Aliwadhihaki marafiki zake, majirani, watoto wadogo na hata wageni kwa maneno yake ya kuumiza. Jambo hili liliwahuzunisha sana wazazi wake.

Alipozungumza, nyakati fulani alisahau kudhibiti hasira yake na kuchagua maneno yasiyofaa. Alipochukia jambo fulani, hangeacha maoni yake makali. Zaidi na zaidi ya marafiki zake na majirani walianza kumkwepa.

Wazazi wake walianza kutambua hili na walijaribu kumshauri mara kwa mara. Kwa bahati mbaya, majaribio yao yote yalishindwa.

Hatimaye, baba ya mvulana huyo alikuja na wazo. Siku moja, baba yake alimpa begi kubwa la misumari.

Alimwomba mwanawe apige msumari mmoja kwenye uzio kila anapokasirika au wakati wowote anaposhindwa kujizuia. Mvulana huyo aliona ni jambo la kufurahisha lakini aliamua kufuata maagizo ya baba yake hata hivyo. Kwa hiyo, hapo alikuwa. Kukimbilia kwenye uzio wa nyuma ya nyumba na kugonga msumari kila wakati alipokosa hasira.

Hasira yake ilimfanya apige misumari 30 kwenye uzio, siku ya kwanza tu! Licha ya kuwa mvulana mwenye hasira, alikuwa mtu mwenye nia na umakini, kwa hiyo alitekeleza maagizo kwa uangalifu kila siku.

Hata hivyo, ndani ya wiki moja, idadi ya misumari iliyopigwa kwenye uzio ilipungua hadi nusu kwa sababu mvulana huyo alikuwa amechoka na ni vigumu sana kupiga misumari mara kwa mara. Aliamua kudhibiti hasira yake badala yake kwani hilo lilikuwa rahisi zaidi.

Taratibu, idadi ya misumari iliyopigiliwa kwenye uzio kila siku ilipungua na kupungua na hatimaye siku ikafika ambapo hakuna msumari hata mmoja uliopigiliwa! Ndiyo! Kijana huyo kwa kweli hakukasirika kwa siku nzima!

Siku chache zilipita. Na kijana bado aliendelea kudhibiti hasira yake. Kwa furaha, alimweleza baba yake jinsi ambavyo hakuwa akipigilia msumari wowote kwani hakupoteza hasira. Baba yake, bila shaka, alifurahiya sana. Sasa alimwambia mwanawe seti mpya ya maagizo. Alimwambia mvulana huyo aondoe misumari 30 kila mwisho wa siku ambayo hakukasirika. Kwa kutaka kujua, mvulana huyo alitii.

Siku kadhaa zilipita na mvulana aliweza kung'oa misumari mingi kutoka kwenye uzio, isipokuwa michache ambayo ilikuwa ngumu sana kuiondoa. Alishiriki ugunduzi huu na baba yake na wote wawili wakaenda nyuma ya nyumba.

Baba yake alimwuliza mvulana huyo, akionyesha uzio, “Unaona nini mwanangu?”

“Uzio wenye mashimo mengi ndani yake. Na kwa kucha chache ambazo haziwezi kuondolewa hata nilijaribu sana,” akajibu.

“Ndiyo mwanangu. Unaona, misumari ni kama maneno yako mabaya, hasira ya kutisha, na tabia mbaya. Waliwekwa kwenye mioyo ya watu unapoumiza hisia zao. Unaweza kuondoa misumari mingi lakini mashimo na mikwaruzo kwenye uzio haiwezi kufutwa. Misumari michache hata imekwama. Hawawezi kutolewa nje kwa vile wamejipachika kwa kina sana kwenye uzio. Watabaki huko sasa kabisa. Uzio hautawahi kuonekana sawa tena.

Kwa hivyo, tunapaswa kuwa waangalifu kila wakati kwa kile tunachosema na kufanya kwa watu. Maneno mabaya ni kama misumari inayochoma mioyo ya watu na kuacha alama hata ikiwa imeondolewa. Maneno mengine yasiyo ya fadhili yanaweza, kwa bahati mbaya, kuwa yamefungwa sana katika mioyo ya watu. Haiwezi kufutwa. Kwa hiyo, mwanangu. Hebu tujaribu kuchagua maneno na vitendo vyetu kwa uangalifu wakati wote, insha Allah.”

.

Maadili:

Kuwa mpole unaposhughulika na watu wengine

Fikiri kabla ya kusema na kutenda

Kudhibiti hasira yako ni hatua ambayo inaweza kufikiwa na kila mtu

TAFUTA MANENO

Yatafute maneno hapo chini kwa kuyazungushia na Penseli

mahari	ukorofi	taawili	sihiri
vurugu	kitendawili	fanaka	ulaghai
hasidi	maktaba	jannataini	tanzim
kiambato	njozi	yakini	khuddam
kiwambo	kitongoji	kaditama	mazingira
barabbara	jangwani	vimbiwa	uaminifu

Y	D	T	N	J	V	I	M	B	I	W	A	K	W	M	K	T	R	M
N	J	O	Z	I	G	N	N	H	L	T	W	A	I	M	J	B	N	D
B	A	R	A	B	B	A	R	A	M	K	B	R	R	J	T	Y	C	C
K	H	U	D	D	A	M	W	I	D	A	A	K	J	M	L	R	Q	X
N	L	L	P	J	C	X	Z	L	T	H	R	I	A	W	V	Y	Y	F
W	C	M	B	G	A	N	J	K	A	K	Z	A	N	K	C	A	X	Z
N	Z	N	H	N	A	N	A	M	A	D	G	M	G	I	T	K	V	V
T	V	M	N	T	M	M	N	M	B	N	N	B	W	T	F	I	Z	L
L	M	K	H	K	D	H	A	A	H	M	X	A	A	E	J	N	F	M
C	Y	L	X	G	I	T	A	N	T	N	W	T	N	N	L	I	J	A
U	R	Q	N	C	I	T	O	S	H	A	N	O	I	D	U	W	Y	Z
C	K	C	S	D	N	B	O	U	I	L	I	I	X	A	L	R	X	I
H	Q	O	A	I	M	M	F	N	M	D	L	N	L	W	A	P	M	N
V	M	K	R	A	H	I	Q	G	G	I	I	N	I	I	G	D	L	G
P	T	K	W	O	N	I	K	D	W	O	M	V	H	L	H	V	R	I
N	Q	I	N	I	F	C	R	A	Z	G	J	D	T	I	A	K	C	R
F	K	H	M	H	Q	I	A	I	Z	P	Y	I	B	G	I	H	B	A
C	K	A	K	T	K	T	M	M	M	F	F	A	N	A	K	A	X	T
D	U	J	W	Z	P	K	V	U	R	U	G	U	N	K	T	R	P	Z

UNGANISHA NUKTA

Unganisha nukta ili upate picha moja iliyokamilika.



Jinsi ya kupika Kababu za nyama ya kusaga

Na **Mtandao**



MAHITAJI

1. Nyama ya kusaga Kilo 1
2. Kitunguu saumu na tangawizi iliyosagwa Kijiko 1 cha chai
3. Pilipili mbichi iliyosagwa kijiko 1 cha chai
4. Bizari ya Kababu ½ paketi
5. Chumvi kiasi
6. Mafuta kiasi ya kukaangia
7. Mayai 2
8. Slice 2 za Mkate

JINSI YA KUPIKA

1. Weka nyama Yako katika bakuli kubwa
2. loweka slice za mkate katika maji kisha zikamue maji uzivuruge kwa mkono ndani ya nyama hakikisha zinachanganyika na nyama vizuri
3. Changanya nyama pamoja na viungo vyote katika bakuli.
4. Chukuwa mayai yako vunjia katika huo mchanganyiko changanya tena mpaka vichanganyike
5. Fanya madonge shape ya duara kama kwenye picha weka kando.
6. Kisha Kaanga kama sambusa mpaka Zibadilike rangi.
7. Epua zikiwa tayari kwa kuliwa.

TANGAZO LA IJTIMAA YA MAJLIS KHUDDAMUL AHMADIYYA TANZANIA

Tanzim ya Khuddamul Ahmadiyya Tanzania inapenda kuwataarifu Khuddam na Atfal wote nchini kuwa Ijtimaa yao itakuwa tarehe 24-26 Juni 2022, Kitonga, Wilaya ya Ilala, Dar es Salaam.

In-Shaa-Allah.

Khuddam na Atfal wote wanaombwa kuendelea na maandalizi ya Ijtimaa hii na kuichangia pia sawa na matakwa ya katiba.

Usipange kukosa!

Limetolewa na Afisa Ijtimaa
Majlis Khuddamul Ahmadiyya Tanzania



Mzee Rashid Msabaha - Sehemu ya I

Huyu alikuwa ni mtoto wa Chifu kutoka milima ya Uluguru mjini Morogoro.

Katika kutafuta taarifa zinazohusu elimu yake, sikuambulia ila mistari michache isiyoweza kuandikwa hata robo ya ukurasa. Lakini thamani na uzito wa mistari hiyo juu ya elimu yake, inashinda thamani ya Lulu na yakuti, fedha na dhahabu iwapo vitawekwa katka mzani mmoja.

Katika mahangaiko ya kutafuta elimu,Mzee Msabaha, alitoka Morogoro hadi Bagamoyo kwa miguu kwenda kwa sheikh Mohammed Ramiya kujifunza elimu ya dini.

Baadaye alifika Kilwa na vitongoji vyake kwa madhumuni hayohayo. Na mwisho, kabla hajajiunga na Jumuiya ya waislam wa Ahmadiyya, alikuwa ni mwanafunzi wa Sheikh Idrisa na Sheikh Hashir, ambao walikuwa ni Masheikh wakubwa na maarufu, si Dar es Salaam tu bali walijulikana pwani na bara ya Afrika Mashariki.

Baada ya kujiunga na Jumuiya katika miaka ya khamsini, alijifunza elimu ya dini, lugha ya kiarabu na kiurdu kwa Maulana Sheikh Muhammad Munawwara na Sheikh Amri Abed kaluta

Mwalim Abdullah Mbanga aliniambia kuwa, Mzee Msabaha alikuwa na ghera kubwa ya kutafuta elimu. Daima alitaka kujifunza hata kwa mtu ambaye kwa maoni ya wengine hajui lolote. Alikuwa ni mkuu wa maktaba pale Masjid Salaam Mnazi mmoja.

Nyumbani kwake alikuwa na nusu ya chumba cha vitabu. Na hiyo ni baada ya kuvichoma nusu vitabu hivyo pindi alipojiunga na Jumuiya, kwa sababu vilikuwa ni vitabu vya uganga wa ramli na talasimu.

Aliagiza kuwa, akifariki, vitabu vyake vipelekwe msikitini pale Mnazi Mmoja.

Alipofariki, mtoto wake akaazimia kuviuza. Wakati anavipeleka sokoni, alipofika Manzese Msufini akapata ajali. Wahuni wakavinyang'anyia, na hivyo hakuambulia hata kitabu kimoja.

Mzee Rashid Msabaha, Alikuwa anafanya kazi katika shirika la Reli katika kitengo cha simu za upepo.(Telegraphist) Hii inaonesha wazi kuwa, kufanya kazi hii katika miaka hiyo, ni wazi kabisa hakukimbia umande katika kujipatia elimu ya ya kawaida.

Itaendelea Inshallah

Siratul Nabi Dar es salaam

Kutoka uk. 1

Mtukufu Muhammad s.a.w alitabiriwa kutoka zama za Nabii Adam a.s. na hivyo ujio wake ulitabiriwa na vitabu vingi kama vile Taurati injili na vingine vingi na hatimae Quran Tukufu imekamilisha utukufu wake.

Baada ya maelezo mafupi ya Mwl Nasoro Kisusa Mwl Habibu alikaribishwa kusoma Shairi la kiurdu.

Na baada ya hapo Rais wa Mkoa aliongea machache kuhusu shughuli na kumjulusha kuwa mahudhurio ya matawi yote manne ni pamoja na lajna. Na hatimaye kumkaribisha Amir na Mbashiri mkuu ambaye aliongea juu ya sifa za Mtume Mtukufu Muhammad s.a.w.

Amir sahib alianza kwa kueleza sifa za Mtume s.a.w alisema kuwa mwenyezi mungu amesema kuwa kama sio Mtume Mtukufu Muhammad s.a.w kufika duniani basi na dunia asingeiumba. Kwa hiyo umuhimu wa Mtume s.a.w ni lazima tujue na kila mara tumsalie sana na ndiyo maana ya kufanya Siratul Nabii. Na jukumu letu kubwa ni kusoma sana vitabu ili tupate kufahamu sifa zake. Na pia tujue jukumu letu kubwa ni kutoa elimu.

Mtume Mtukufu s.a.w ni mfano kamili kwa ajili yetu, na kumfuata yeye ndiyo mafanikio yetu. Kila kitu kimeelezwa kwenye Quran Tukufu. Imeelezwa kwenye hadithi zake Na pia imeelezwa kwenye sunna zake.

Aliongeza kusema kwamba ni masikitiko makubwa kuwa baadhi ya watu wengine wanashindwa kueleza ukweli wa Mtume s.a.w hasa nchi za ulaya ambao wanajaribu sana kuharibu sifa zake Mtume Mtukufu Muhammad s.a.w na kutoa maelezo ya uongo ulimwenguni kumhusu yeye

Wakristo Nao wanashindwa kuona utukufu wa mtume s.a.w na kutoa kauli tofauti na sifa zake.

Amir sahib al…

MATUKIO KATIKA PICHA









Qaideen Forum 2022





Mkutano kuhusu "Sira ya Mtume Muhammad" Mtukufu Zanzibar, Tanzania

Kambi ya Malezi ya Vijana wa Wilaya Ushetu, Shinyanga







Ufunguzi wa Masjid Bait-ul-Ghafoor, Mpanda









Mahafali ya Jamia Ahmadiyya Tanzania 2021







Umuhimu, Ubora na Fadhila za kumsalia Mtume*saw*



Na **Sheikh Karimuddin Shams**
Mbeya, Tanzania

Dua muhimu sana mno, inayopokelewa moja kwa moja na kuleta baraka na heri nyingi kwa ajili ya mwombaji ni sala ya mtume saw yaani kumsalia Mtume Mtukufu saw. Nasi tumehimizwa ndani ya Qurani Tukufu kuhusu jambo hili. Mwenyezi Mungu Anasema:

اِنَّ اللّٰهَ وَمَلٰٓئِكَتَهٗ يُصَلُّوْنَ عَلَى النَّبِيِّ.يٰٓاَيُّهَاالَّذِيْنَ اٰمَنُوْا صَلُّوْاعَلَيْهِ وَسَلِّمُوْاتَسْلِيْمًا ۔

kwa yakini Mwenyezi Mungu na Malaika wake wanamsalia Mtume saw. Enyi mlioamini! Ninyi nanyi msalieni (kumsalia Mtume saw ni kumwombea dua ya kupata rehema, baraka na amani) na mwombeni amani sana. (Sura Alahzab 33:57)

Maana ya sala kuzipitia aya za Kurani Tukufu

@@@@@@@@@@@@@@@ @@@@@@ ni neno la kiarabu liliotumika ndani ya aya iliyotajwa hapo juu na neno hili lina maanisha kama yafuatayo kuzipitia aya zingine za Qurani Tukufu:

هُوَالَّذِيْ يُصَلِّيْ عَلَيْكُمْ وَ مَلٰٓئِكَتُهٗ۔۔ (A l - ahzab:44)

Yeye ndiye anayewarehemuni na Malaika Wake pia. (Tafsiri ya Hazrat Mirza Tahir Ahmad rh.)

اُولٰٓئِكَ عَلَيْهِمْ صَلَوٰتٌ مِّنْ رَّبِّهِمْ وَ رَحْمَةٌ۔۔ (Al-Baqarah:158)

Hao ndio, ziko baraka na rehema juu yao kutoka kwa Mola wao. (Tafsiri ya Hazrat Mirza Tahir Ahmad rh.)

اِنَّ اللّٰهَ وَمَلٰٓئِكَتَهٗ يُصَلُّوْنَ عَلَى النَّبِيِّ۔۔ (Al-Ahzab:57)

Kwa yakini Allah na Malaika wake wanamtakia rehema Mtume saw. (Tafsiri ya Hazrat Mirza Tahir Ahmad rh.)

Maana ya kiistilahi na ya Kilugha

Hazrat Mirza Bashir Uddin Mahmood Ahmad r.a. khalifa wa pili wa seyyedna Ahmad a.s. anasema akieleza neno la sala kwamba:

Maana ya صلَّ ، يصلِّ ni kuomba dua na maana yake ya kiistilahi ni ….kuomba dua kwa kufuata mfumo ule unaojumuisha ndani yake Rukuu na Sujda…kisha kuna maana zingine pia zipo ambazo haziko bure bali zote zinaelekeza kwenye ukweli mmoja tu hivyo maana zingine ni kama zifuatazo: rehma, sheria, ghofira, kuomba, dua, kudhihirisha ukubwa, baraka…..

na neno sala litumikapo kwa ajili ya Allah Mtukufu humaanisha kurehemu na litumikapo kwa ajili ya Malaika humaanisha ghofira, na litumikapo kwa ajili ya waaminio huleta maana ya dua au sala (inayosaliwa mara 5 kwa kutwa) na litumikapo kwa ajili ya ndege au wadudu humaanisha kutukuza. Neno la salat linatumika kwa ajili ya dua njema tu ila neno la dua linatumika kwa maana zote mbili za dua njema na dua baya. Na maana moja wapo ya salati ni kumsifu mno mtume saw kutoka kwa Allah Mtukufu. (Tafsire Kabiir J.1.UK.98)

Hazrat Masih ul Maud a.s. anasema akitufanulia hili kuwa: Darood (sala ya mtume saw katika kiajemi) limetokana na dard(maumivu) yaani kumuomba Mwenyezi Mungu kwa hamu, huzuni, maumivu na uyenyekevu mkubwa mno kwamba E, Mola! Mpe Mtume Mtukufu saw neema maaluma na madaraka makubwa yenye heshima na taadhima kubwa mno kutoka kwetu. Tuwezaji kufanya nini na kwa namna ipi kumlipia juu ya hesani zake? Isipokuwa tukuombe Wewe tu ili Umpe malipo ya kweli kutokana na juhudi na kazi zake kubwa mno Uliyoandaa kwa ajili yake saw. Mtu anapoomba dua kwa moyo wa huzuni, maumivu na uyenyekevu mkubwa wa namna hii kwa ajili ya mtume saw basi madaraja yake mtume saw huyanyuliwa na kushushiwa rehema maalum kisha mwombaji huyu anayemsalia mtume saw pia anateremshiwa rehema kutoka huku na kupewa ujira mara kumi juu ya sala (dua) hiyo. (Al-Hakam ya Aprili 6, mwaka 1908).

Sala ya mtume saw ni kitu cha kukiweka kipau mbele kwa ajili ya kukubaliwa kwa dua. kisha ni muhimu sana kutafuta njia ya kupata ukaribu na Allah mtukufu ambayo ni kumsalia sana mtume saw ili maombi yetu yakubaliwe zaidi kwani imeelezwa katika hadithi za mtume saw kwamba dua inayojijumuisha dua za kila namna ni sala ya mtume saw halafu mwanzilishi mtukufu wa jumuiyya ya Waaislam Waahmadiyyah hazrat Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian a.s. ametusisitizia sana juu ya kumsalia sana mtume saw.

Khalifa wetu mpendwa hazrat mirza Masroor Ahmad a.t.b.a. anasema akieleza ukweli huu kwamba:

Sala ya mtume saw ni kitu muhimu zaidi kwa ajili ya kukubaliwa kwa maombi. Hazrat Masih e Maud a.s pia ametulielekeza na imebainishwa katika hadithi za Mtume Mtukufu*saw* pia na juu ya hayo yote Mungu Mwenye Enzi Mwenyewe Amesisitiza kuhusu hilo ndani ya Kurani Tukufu hivyo tunatakiwa kulielekea kama kwaida. Kama alivyoelekeza kuhusu hilo hazrat khalifa tul Masih wa nne akitangaza mpango maalum basi nami pia naikumbusha tena kwamba tumsalie sana mno mtume saw ndani ya mwezi huu (wa Ramadhan)…pia hii ndio njia bora zaidi ya kudhihirisha upendo wetu kama wapendwa wa mtume saw na italeta baraka za namna nyingi kwa ajili ya kuyatimizia makusudio ya hazrat Masih e Maud a.s.aliye ni ashiki wake wa kweli wa Mtume saw. Inshaa Allah Taalah.

(Khutbat e Masroor J.8.uk.636)

Tunapata kuelewa vyema zaidi kupitia hadithi za Mtume mtukufu s.a.w pamoja na maelezo ya seyyedna Ahmad a.s. kwamba, sala ya mtume saw ni dua inayojijumlisha maombi ya kila namna ndani yake kisha hiyo ni dua inayopelekewa moja kwa moja na kukubaliwa mno, hivyo ningependa kuweka mbele ya wasomaji wetu baadhi ya hadithi za Mtume s.aw. na nukuu za hadhrat Ahmad a.s.

Njia nzuri ya kupokelewa kwa dua

Hazrat Mufti Muhammad Sadik r.a. sahaba wa Seyyedna Ahmad a.s. anatusimulia akisema:.. siku moja nilipokuwa nimekuja Qadian na kukaa na Hazrat Ahmad a.s.kwenye msikiti wake “Masjid Mubarak” nilisema kwamba huzur ninatumai kuwa, nimwombe Mwenyezi Mungu kuipitia sala ya mtume s.a.w.tu kuliko kuomba maombi mengine mengine. Seyyedna Ahmad a.s. alilipenda na kuniombea dua kwa kuyanyua mikono yake yote miwili mbele ya wahudhurio wote. Ndipo toka muda huu ninaomba maombi yangu yote kwa kujiingiza katika sala ya mtume s.a.w. na nimeshuhudia kuwa njia hii ni nzuri mno ya kupokelewa kwa maombi…

(Mufti Muhammad Sadik r.a.)

Tukoi la namna hii limesimuliwa na Hazrat Ubayyi bin Ka’ab r.a pia anayesimulia hivi kwamba, Yeye anasema: Mimi nilimuelezea Mtume saw kuwa, natumia sehemu kubwa ya maombi yangu katika kumsalia Nabii saw na ni bora kama Huzur saw mwenyewe aniambie kuwa, nitumie muda gani kati ya muda wa maombi yangu katika kumsalia Nabii saw. Mjumbe saw alisema kadri unavyopenda. Nilisema je, robo ya muda? Alijibu jinsi unavyotaka, kama unaweza kuuzidisha basi itakuwa bora zaidi kwako. Nilimuuliza je, nusu ya muda? Alisema jinsi upendavyo, na kama unauongeza basi ni bora zaidi. Nilimuomba je, thuluthi mbili? Alijibu jinsi uwezavyo, kama utaongeza humo basi itakuwa bora kabisa. Nilisema naweka muda wote wa maombi yangu kwa ajili ya kumsalia Mtume saw. Mtume saw alisema basi ndipo taabu na huzuni yako yote yataondoka kwako na madhambi yako yote yatasamehewa.

(Tirmizi Abwab sifa ya Kiyama)

Yaani sala ya mtume saw ni chanzo bora kabisa kwa ajili ya kuondoa shida, taabu na huzuni ya kila namna pamoja na kupata msamaha wa madhambi.

Imam uz zaman hazrat Aqdas Masihe Maud a.s. ameeleza mfano wake wa dhati kwa maneno yafuatayo kuwa:

ہرکسے اندرنمازخوددعائےمیکند۔من دعاہائےبروبارتواے باغ وبہار

Tafsiri: watu wanaomba dua kwa ajili ya manufaa zao za dhati ndani ya sala lakini mimi ninaomba dua juu ya makusudio ya mtume saw na ili madaraja yake yapate kuyanyuliwa kila siku.

Fadhila na ubora wa Kumsalia Mtume saw

Sasa ningependa kuweka mbele ya wasomaji wetu baadhi ya hadithi zingine za bwana wetu Mtume s.a.w. kuhusu umuhimmu na baraka za kumsalia Mtume s.a.w.

Mtume Mtukufu saw anasema: anisaliaye mara moja basi Mwenyezi Mungu Atamshushia rehema kumi. (Sahih Muslim)

Seyyedna Ahmad a.s. anasema;

گرخواہی کہ حق گوید ثنایت۔ بشنوازدل ثناخوان محمد

Yaani kama unataka upate kusifiwa na Mungu Mwenye Enzi basi uwe mwenye kumsifu na kumsalia Mtume s.a.w. kwa moyo wote.

Imesimuliwa na Hazrat Abdullah bin Omar r.a. kwamba:

Yeyote atakayemsalia mtume s.a.w. mara moja (kwa uaminifu) basi Mwenyezi Mungu na Malaika Wake watamsalia mara 70 hiyo akipienda anaweza kuongeza idadi hii ama kupunguza.

(Jilaul Ifham kwa kumbukumbu ya Musnad Imam Ahmad)

imesimuliwa na Hazrat Aamir bin Rabiah ra ya kwamba Mtume saw alisema: “Mwislamu yeyote anisaliaye, basi Malaika huendelea kumsalia kwa wakati wote atakao kuwa ananisalia. Sasa akipenda anaweza kuzidisha. (Jilaul Ifham)

Kutafuta radhi ya Allah kupitia kujitolea kifedha na Tangazo la mwaka wa 65 wa Waqf-e-Jadid

Kutoka uk. 12

Leone 100,000. Yeye akamhimidi Mwenyezi Mungu na kusema kuwa walikuwa wamepungukiwa katika ahadi zao za Waqfe Jadid, na pindi walipoomba akaja huyo mtu na kumpa hizo pesa.

Khalifa mtukufu*atba* alisema kwamba mifano hiyo pia inapatikana miongoni mwa kinamama.

Mtukufu Khalifa*atba* alisema kwamba kulikuwa na mwanamke nchini Chad, ambaye alikuwa ameahidi Faranga 70,000 kwa ajili ya Waqf-e-Jadid, hata hivyo hakuweza kujiwekea fedha za kutimiza ahadi hiyo. Hivyo, aliuza ngamia aliokuwa nao kwa Faranga 170,000. Alitumia fedha hii kutimiza ahadi yake, lakini hakujiwekea kiasi kilichobaki, bali aliwasilisha kama mchango wa kifedha pia.

Mtukufu*atba* alisema kwamba mifano kama hiyo inapatikana pia miongoni mwa vijana. Khalifa mtukufu*atba* alisema kwamba Belize ni sehemu katika Amerika ya Kati, ambayo ni mbali sana, na Khalifa hajawahi kwenda huko. Wote ni wanajumuiya wapya, lakini mawazo yao ya kujitolea ni sawa tu. Hapo, mvulana wa miaka 14 ambaye alikuwa ametoa mchango kwa ajili ya Tehrik-e-Jadid alitajwa katika hotuba ya Ijumaa na Khalifa mtukufu. Watu wengi walimpongeza, na hata mtu mmoja akampa zawadi ya $200. Watoto wengi wangechukua kiasi kama hicho na kujinunulia vifaa vya michezo. Hata hivyo, mvulana huyu mdogo alisema kwamba alihitaji $30 kutengeneza kadi yake ya hifadhi ya jamii, na kwamba angetoa $170 iliyobaki kama mchango wa kifedha. Anatoka katika kaya maskini, na alihimizwa kujiwekea kiasi hicho. Hata hivyo, alikuwa thabiti katika uamuzi wake. Khalifa mtukufu*atba* alisema kwamba huu ni mfano ya kutanguliza imani juu ya dunia. Aliomba kwamba Mwenyezi Mungu adumishe fikra hii ndani ya kijana huyu mdogo na amuepushe na athari za dunia.

Khalifa Mtukufu*atba* alisema kwamba mifano hiyo inapatikana katika nchi maskini zaidi. Watu wanaweza kuwadharau watu kama hao kwa sababu hawajasoma vizuri, lakini kwa kweli, watu hawa wana ujuzi zaidi wa imani kuliko watu waliosoma zaidi.

Khalifa mtukufu*atba* alisema kwamba mbashiri katika Guinea-Conakry alitoa mawaidha kuhusu umuhimu wa kujitolea kifedha ambapo pia aliwasilisha nukuu mbalimbali za Khalifa mtukufu*atba*. Mwishoni mwa hotuba yake, mtu ambaye alikuwa maskini kabisa lakini mkweli sana alichukua Faranga 218,500 kutoka mfukoni mwake na kuzitoa kwa ajili ya Waqf-e-Jadid. Wakati mbashiri alipomuuliza kwa nini alikuwa anatoa kiasi kikubwa hivyo, alisema kwamba aliathiriwa sana na maneno ya Khalifa mtukufu*atba*, kwamba moyo hauwezi kupenda vitu viwili kwa wakati mmoja; mtu lazima ama ampende Mwenyezi Mungu au apende mali. Alisema kwamba asingeweza kutoa kila kitu cha nyumbani kwake kama Hadhrat Abu Bakr (ra) alivyofanya, lakini angalau angeweza kutoa chochote kilichokuwa mfukoni mwake. Pia alieleza kwamba tangu alipoanza kutoa dhabihu za kifedha, aliona kwamba Mungu alikuwa ameongeza imani na yakini yake.

Khalifa mtukufu*atba* alisema kwamba watu katika nchi zilizoendelea pia wana roho hiyo hiyo ya kujitolea. Mbashiri mmoja nchini Ujerumani aliwahimiza Wanajumuiya waongeze bidii yao ya kifedha. Mwanamke wa Kijerumani ambaye alibadili dini kuwa Ahmadiyya muda mrefu uliopita aliwasilisha Euro 19,000. Alisema kwamba ingawa alikuwa akiweka akiba kiasi hiki ili kununua gari, alisema kwamba angependelea zaidi kupata radhi za Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Khalifa mtukufu*atba* alisema kwamba mtu kutoka Uingereza alipokea barua kutoka Halmashauri ya jiji kumjulisha kwamba alikuwa na deni la malipo ya huduma ambayo hayajalipwa. Pia alikuwa amepokea simu kuhusu malipo ya ahadi yake ya Waqf-e-Jadid. Aliamua kwamba angelipa kwanza ahadi yake kwa ajili ya Waqf-e-Jadid. Siku iliyofuata alipokea barua nyingine kutoka baraza la madiwani ikieleza kuwa wamekosea, na badala ya kumdai yeye, wakagundua ukweli kuwa yeye ndiye alikuwa anawadai wao. Kisha wao wakamtumia kiwango cha pesa ambacho kilikuwa zaidi ya malipo yake ya Waqfe Jadid mara kumi.

Kisha Hadhrat Khalifatul Masih*atba* alisimulia tukio moja kutoka Tanzania kwamba: Mwalimu wetu, Chande Nyenje kutoka Jamat ya Mwang›alanga, Shinyanga, Tanzania anaandika:

“Tawi hili ni jipya kabisa. Kuna ndugu yetu kutoka hapo mzee Ramadhan Andrea alijiunga na Jamaat mwaka mmoja uliopita. Tulipoanza kuingiza nidhamu ya Jamaat kwenye mioyo yao tulipata shida kidogo kueleweka hasa nidhamu ya michango. Lakini mzee huyu mkulima alianza kuweka ahadi ya Tahrik Jadid na Wakfu Jadid ambazo alilipa mara mbili ya ahadi yake. Nikiwa katika malezi ya wanajamat na kusisitiza baraka za kujitolea mali, mzee huyu alikitoa kiwanja chake, mali ya familia yake kuipatia Jamat. Jambo hili lilizusha mshangao mkubwa kwa watu wa kijijini kwake, sababu kwa uchanga wao katika Jamat wasingefikiria hatua hiyo. Wengi walim’beza sana mzee huyo kwamba anamaliza mali, eti kwa ajili ya dini tu, atakuwa amelogwa, sio bure.

Mwalimu anaendelea kuandika: Mimi pia mwanzoni nilihofia kwamba atabdilika lakini mwenyewe aliondoa hofu yangu. Siku moja alimwita mke wake na mwanaye mmoja, majirani na wazee wa mtaa wanajamat na serikali ya mtaa na kutamka kuwa amekitoa kiwanja chake kwenye Jamat kama shukrani yake kwa Allah. Akaendelea kusema mimi sikujua umuhimu wa kutoa katika njia ya Allah mpaka nilipojiunga na Ahmadiyya. Sasa nalipa michango yangu hasa Tahrik Jadid na Wakfu Jadid. Akasema, uongo ni dhambi, maisha yangu yameimarika sana. Nimenunua viwanja maeneo mbalimbali zaidi ya hiki nilichokitoa na mwaka huu nimejenga nyumba na zimekamilika nyumba mbili. Akasema, mimi naona na nakiri kuwa haya yote yamewezekana kwa sababu Allah Anayabariki, na mimi sijafanya chochote tofauti na ninyi isipokuwa najitahidi sana sawa na uwezo wangu kulipa michango yangu. Akasema nimewaita muwe mashahidi tu, mimi sijalogwa na sina upungufu wa akili.

Mwalimu anamalizia kuandika; tukafanya yanayostahili kuimilikisha Jamat kiwanja hicho na hapo hapo akaniambia kuwa na mwaka huu ahadi yake ya Tahrik Jadid na Wakfu Jadid ni mara mbili ya ile ya mwaka jana.»

Mafanikio Mbalimbali ya Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya mwaka 2021

Khalifa Mtukufu*atba* alisema kwa kutaja kujitolea kifedha kwa ajili ya kueneza imani, anapenda kutaja kwamba katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita, Mwenyezi Mungu aliiwezesha jumuiya duniani kote kujenga misikiti 187, hiyo ni mbali na misikiti 105 inayoendelea kujengwa barani Afrika. Vile vile, nyumba za wabashiri 144 zilijengwa, nyingi zikiwa barani Afrika, wakati 45 zinaendelea kujengwa. Mahali ambapo nyumba za wabashiri haziwezi kujengwa, majengo yanapatikana kwa kukodisha; kwa hivyo kuna nyumba 731 za wabashiri ambazo zinakodiwa barani Afrika. Pia kuna nyumba 632 za wabashiri zinazokodiwa katika nchi zingine za Asia. Khalifa Mtukufu*atba* alitaja kwamba kwa ujumla, kiasi kikubwa cha fedha kinachokusanywa kwa ajili ya Waqf-e-Jadid kinagawiwa kwa nchi za Kiafrika.

Khalifa Mtukufu*atba* alisema kuwa kujenga misikiti si jambo jepesi, kwani Jumuiya yetu inapaswa kukabili upinzani mkubwa. Hata hivyo, kwa sababu jumuiya yetu inafanya mambo haya kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, Yeye pia hutoa msaada Wake. Kwa mfano, msikiti ulikuwa unajengwa Kongo-Kinshasa. Hapo, Waislamu wa Kisunni walileta matatizo mengi na wakajaribu kuzuia ujenzi wa msikiti huu, na wakati juhudi zao ziliposhindwa, walianza kutoa vitisho vya kifo. Pamoja na hayo, ujenzi wa msikiti uliendelea. Siku moja, profesa Mkristo kutoka chuo kikuu cha hapo alikuja na kuanza kuwasaidia Waahmadiyya katika kujenga msikiti. Kwa hiyo, pale wapinzani walipokuwa wakijaribu kuzuia ujenzi wa msikiti huo, Mwenyezi Mungu alileta watu wengine kusaidia katika kuukamilisha.

Hii ilikuwa ni baadhi tu ya mifano ya iliyotolewa na Khalifa mtukufu*atba*.

Ripoti ya mwaka 2021 na Tangazo la Mwaka wa 65 wa Waqf-e-Jadid

Khalifa Mtukufu*atba* alisema kwamba angewasilisha ripoti ya mwaka uliopita kwa ajili ya Waqf-e-Jadid.

Kwa fadhili ya Mwenyezi Mungu, mwaka wa 64 wa Waqfe Jadid uliisha, na mwaka mpya umeanza. Katika mwaka uliopita mchango wote wa Waqfe Jadid ulikuwa Paundi milioni 11.2. Hiyo ni nyongeza ya Paundi 742,000 (fedha ya Uingereza) kutoka mwaka uliokuwa kabla yake. Tunapoona hali mbaya ya dunia siku hizi, haya ni mafanikio makubwa sana.

Hadhrat Khalifatul Masih Wa Tano*atba* alisema kuwa kulingana na mchango wa mataifa yote. Jumuiya ya Uingereza imeshika nafasi ya kwanza, kisha Ujerumani, Kanada, Marekani, India, Australia, Indonesia, taifa moja la Mashariki wa kati, Ghana na Ubelgiji.

Kwa chi za Afrika ya kwanza ni Ghana, kisha Mauritius, Nigeria, Burkina Faso, Tanzania, Sierra Lione, Liberia, Gambia na Uganda.

Hadhrat Khalifatul Masih Wa Tano*atba* alitoa taarifa ya nafasi za mbele ya maeneo ya mataifa yaliyoongoza duniani.

Hadhrat Khalifatul Masih V*atba* aliomba kuwa Mwenyezi Mungu Awabariki wale wote waliojitolea kifedha. Amin.

The First Muslim Newspaper in Swahili Language since 1936

MapenziyaMungu

SAFAR - JAM.I 1443 AH | JANUARI 2022 | TAB.-FAT 1400 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu[saw]

Imesimuliwa na hadhrat Ibn Umar[ra] ya kuwa: Mtume[saw] alisema: "Msijihusishe katika mazungumzo mengi isipokuwa yanayohusika na kumkumbuka Allah. Maana kuzungumza sana bila ya kumtaja Allah huufanya moyo kuwa mgumu! Na mtu aliye mbali sana na Allah ni mwenye moyo mgumu" (**Tirmidh**)

Kutafuta radhi ya Allah kupitia kujitolea kifedha na Tangazo la mwaka wa 65 wa Waqf-e-Jadid

Katika hotuba ya Ijumaa iliyotolewa Masjid Mubarak tarehe 07/01/2022; Baada ya Tashahhud, Ta'awwudh na Surat Faatihah, Khalifa Mtukufu V, Hazrat Amir ul Momeniin, Mirza Masroor Ahmad[atba] ('Ayyadahullahu Ta'ala Bi-Nasrihil Aziiz') alisoma aya ifuatayo:

وَمَثَلُ الَّذِيْنَ يُنْفِقُوْنَ اَمْوَالَهُمُ ابْتِغَآءَ مَرْضَاتِ اللّٰهِ وَتَثْبِيْتًا مِّنْ اَنْفُسِهِمْ كَمَثَلِ جَنَّةٍۢ بِرَبْوَةٍ اَصَابَهَا وَابِلٌ فَاٰتَتْ اُكُلَهَا ضِعْفَيْنِ ۚ فَاِنْ لَّمْ يُصِبْهَا وَابِلٌ فَطَلٌّ ؕ وَاللّٰهُ بِمَا تَعْمَلُوْنَ بَصِيْرٌ ﴿۲۶۶﴾

Na mfano wa wale wanaotoa mali zao kwa kuitafuta radhi ya Allah na kujiimarisha wenyewe, ni kama mfano wa bustani iliyo mahali pa juu, ikaifikia mvua kubwa na ikaleta matunda yake mara dufu; na ikiwa haifikiwi na mvua kubwa basi hata umande (huitoshea); na Allah Anayaona mnayoyatenda. [Qur'an 2:266].

Khalifa mtukufu[atba] alisema kuwa katika Aya hii, Mwenyezi Mungu Mtukufu anawataja wale waumini wanaotoa katika njia ya Mwenyezi Mungu, ili wapate radhi zake. Kwa kufanya hivyo, wanaiimarisha Jumuiya na kazi zao pia. Khalifa mtukufu[atba] alisema kwamba katika zama hizi, Masihi Aliyeahidiwa[as] alipewa jukumu la kueneza ujumbe wa kweli wa Uislamu ulimwenguni kote, na jukumu hilo hilo liko kwa wafuasi wake. Hivyo, kila mtu lazima awe tayari kujitolea maisha yake, mali na heshima kwa ajili ya kazi hii. Kwa hakika hicho ndicho kipimo cha kweli cha imani ya mtu.

Kupata Radhi ya Mwenyezi Mungu Kupitia Dhabihu za Fedha

Khalifa mtukufu[atba] alisema kwamba waumini wa kweli wanatumia mali zao kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na kueneza ujumbe Wake. Hawafanyi hivyo ili kuwavutia wengine, bali ili kupata radhi ya Mungu, kuimarisha imani yao wenyewe, na kusaidia kuimarisha Jumuiya. Watu wanaotoa dhabihu kama hizo hujaribu kufikia viwango vya juu zaidi, kwa sababu hiyo Mungu hukubali juhudi zao na kuwapa baraka zake. Mungu anajua hali ya mioyo ya kila mtu; Yeye hajali kama dhabihu ya kifedha ni kubwa au ndogo, badala yake anaangalia nia ya mtu.

Umuhimu wa Nia ya Mtu Wakati wa Kutoa Sadaka

Khalifa mtukufu[atba] alisema kuwa Mwenyezi Mungu amewafananisha wale wanaotoa sadaka za fedha na ama mvua kubwa, au mvua ndogo, akimaanisha wale walio na mali wanaweza kutoa kiasi kikubwa, ambapo wale ambao hawana mali nyingi watatoa kidogo. Hata hivyo, yote mawili yana manufaa katika ukuaji wa matunda, kwani hatimaye, Mwenyezi Mungu ndiye anayekuza matunda, na anaona nia ya mtu, ambayo Yeye pekee ndiye anayeweza kuifanya kuwa na matunda. Hivyo, kila jambo tunalofanya lazima liwe kwa ajili ya kumpendeza Mungu.

Khalifa mtukufu[atba] alisema kwamba wakati wa Masihi Aliyeahidiwa[as], wengi wa masahaba wake hawakuwa matajiri sana, lakini walikuwa mstari wa mbele katika kutoa dhabihu za kifedha. Khalifa mtukufu[atba] alisema kwamba shauku na jazba hiyo hiyo inaonekana katika jumuiya ya Masihi Aliyeahidiwa[as] leo. Mifano kama hiyo inapatikana hata kwa wanajumuiya wapya, ambao bado hawajapata maarifa mengi ya imani kama wengine, lakini wameendelea sana katika kiwango chao cha kujitolea. Vivyo hivyo, Jumuiya siku hii ya leo inaamini na kutii Ukhalifa kiasi hiki kwamba, kama alivyosema Hadhrat Masihi Aliyeahdiwa[as] kuwa, hata wapinzani wanashangazwa na kiwango hiki cha upendo. Hadhrat Khalifatul Masih Wa Tano[atba] alisema kuwa katika wakati huu ambapo watu wamezama katika mambo ya kidunia, hao watu wanashindana wenyewe kwa wenyewe katika kujitolea kifedha kwa ajili ya Mwenyezi Mungu tu.

Mifano ya Ajabu ya Waislamu wa Ahmadiyya Wakitoa Dhabihu za Kifedha

Khalifa mtukufu[atba] alisema kwamba atawasilisha baadhi ya mifano ya jinsi wanajumuiya wanavyodhihirisha imani na yakini yao kwa njia ya dhabihu za kifedha, na jinsi Mwenyezi Mungu Mtukufu anavyotoa baraka zake kwa matokeo hayo.

Hadhrat Khalifatul Masih Wa Tano[atba] alisema kuwa kuna sehemu ya mbali katika Siera Leone ambapo mbashiri wetu aliwakumbusha watu kuhusiana na umuhimu wa kujitolea kifedha. Imamu wa msikitini hapo alieleza kuwa hawataweza kufikia lengo lao. Mbashiri wetu akawaongoza katika maombi ya kimya, na kisha akaondoka na kuelekea makazi ya Mbashiri. Kabla hajafika kwenye nyumba ya mbashiri, imam wa eneo hilo alimpigia simu na kumweleza kwamba anakuja kukutana naye. Alipofika, alieleza kwamba baada ya maombi ya kimya-kimya, jamaa yake mmoja alimwendea na kumpa

Endelea uk 11



KITABU

Zawadi kwa Nadwa

"Yawezaje mdai uwongo wa utume afananishwe nami? Nimeungwa mkono na miujiza mingi… Mafanikio yangu yanatoka kwa Mungu na ni utimilifu wa ahadi zake. Haiko ndani ya uwezo wa mwanadamu yeyote."

Kwa ujumbe huu rahisi ndio '*Zawadi Kwa Nadwa*' iliwekwa wakfu. Katika kivutio hiki kifupi na chenye utuvu, Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as] anajibu ubishi uliotolewa na Hafidh Muhammad Yusuf kwamba hata wadai wa uongo wa Utume wanaweza kuanzisha misheni zenye mafanikio. Kwa kutumia ukosoaji huu, Muhammad Yusuf alitarajia kudhoofisha mafanikio ya Masihi Aliyeahidiwa[as]. Kwa hoja zenye nguvu na Madhubuti, Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as] anaivunja nadharia hii na kufichua dosari na kasoro zake sugu. Anajenga hoja kuwa manabii wa uwongo hawawezi kamwe kufaulu na kwamba kushikilia imani hizo ni kupingana na mafundisho ya Uislamu. Badala yake, ushindi wa Mitume wa Mwenyezi Mungu ni muujiza na ishara ya Mwenyezi Mungu katika kuunga mkono ukweli wao. Walengwa wakuu wa kazi hii walikuwa ni maulamaa wa An-Nadwah ambao waliitwa na Hafidh Muhammad Yusuf kuhukumu ubora wa madai haya yanayopingana.

Jipatie nakala yako kwa bei ya maktaba ya Tsh. /=

Kwa Makala, Maoni, Ushauri; Tuandikie

mapenziyamungu36@gmail.com